
Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



## Mbaraka Mwinshehe bado kipenzi cha wana Morogoro
Uk. 22

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00058 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano April 3 - 9, 2024 |



## Sheria Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi sasa rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge Dk. Tulia Ackson, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameisaini miswada ya sheria minne kuwa sheria. **Uk. 2**

## Vivuko maalum barabara ya Mwendokasi



Uk. 5

# Samia kuzitoa kifungoni Bureau de Change nchini

- Ni zile zilizofungiwa miaka 8 iliyopita
- Fedha na mali kurejeshewa wahusika




## Balozi Dk. Nchimbi 'amwagiwa' baraka za Mzee Yusuf Makamba

## Askofu David Mwasota aandika historia Pasaka



**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly Tanzania, Dk. David Mwasota, amewashangaza wengi hususan washirika (waumini) wa kanisa hilo baada ya kuamua kuwapa medali za dhahabu Wachungaji wote wa kanisa hilo Jimbo la Dar es Salaam. **Uk. 5**

UZINDUZI MBIO ZA MWENGE 2024:

## Mafanikio makubwa miaka mitatu ya Samia - Majaliwa



# Balozi Dk. Nchimbi `amwagiwa' baraka za Mzee Makamba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amemtembelea kumjulia hali Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Yusuf Makamba, nyumbani kwake jijini Dar es Salaam.

Balozi Dk. Nchimbi alifanya hivyo juzi ambapo Mzee Makamba alimpongeza kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo na kumtakia heri kwenye majukumu hayo mapya na kumzawadia shati moja la sare ya CCM ikiwa ni ishara ya kifaa cha kazi.

Balozi Dk. Nchimbi, alimshukuru Mzee Makamba kwa zawadi hiyo na kumshukuru.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alipomtembelea Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Yusuf Makamba, kumjulia hali nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana.

# Sheria Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi sasa rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge Dk. Tulia Ackson, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameisaini miswada ya sheria minne kuwa sheria.

Spika Dk. Tulia amesema kwa sasa sheria hizo zitaitwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani namba 1 ya mwaka 2024, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi namba 2 ya mwaka 2024, Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa namba 3 ya mwaka 2024 na Sheria ya Marekebisho mbalimbali ya Sheria namba 4 ya mwaka 2024.

Alisema hayo wakati akilitaarifu Bunge katika Mkutano wa 15 jijini Dodoma jana.

Alisema katika Mkutano wa 14 wa Bunge, wabunge walipitisha miswada minne ya sheria, ambayo sasa imepata kibali rasmi kwa Rais Dk. Samia ili ianze kutumika kwa mujibu wa sheria.

"Kwa taarifa hii napenda kulitaarifu Bunge hili tukufu kuwa tayari miswada hiyo minne imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais Dk Samia na kuwa sheria za nchi," alisema.



Spika Dk. Tulia Ackson)

# Mashirika yabanwa kuwasilisha taarifa, ada

**Na Mwandishi Wetu**

MASHIRIKA yasiyo ya kiserikali, yametakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi zao kwa mwaka 2023 na kulipa ada.

Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Mashirika hayo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Vickness Mayao, mwisho wa kulipa ada na kuwasilisha taarifa ni Aprili 15.

Alisema baada ya muda huo mashirika yatakayoshindwa kutekeleza kwa wakati malipo yote ya ada yataliwa na faini.

Alisema baada ya Aprili 16, mwaka huu, mashirika yote ambayo hayajawasilisha taarifa na kulipa ada yatatangazwa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Tovuti ya Wizara.

Msajili wa Mashirika hayo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Vickness Mayao





Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel

# 'Bima ya Afya suluhu utekelezaji Sera ya Wazee'

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya imesema kuanza kwa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote, itakuwa suluhu ya kudumu ya utekelezaji wa Sera ya Wazee kupata matibabu bure kila Kituo cha Afya nchini.

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, alisema hayo kwenye Bunge la 12, Mkutano wa 15 na Kikao cha Kwanza wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maakum Tauhida Gallos aliyetaka kujua kama Sera ya Wazee kupata matibabu bure inatekelezwa katika kila Kituo cha Afya nchini

"Wazee wasio na uwezo wa kugharimia huduma za afya, wameendelea kupatiwa huduma hizo kwa utaratibu wa msamaha, hata hivyo, ni kweli kuna changamoto kwenye baadhi ya maeneo," alisema.

Dk. Mollel alitoa wito kwa wabunge na madiwani, kuhakikisha wanashirikiana ili kusimamia Sera ya Wazee kupata matibabu bure inatekelezwa katika maeneo yao ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sera hiyo katika maeneo yao.

**Wazee wasio na uwezo wa kugharimia huduma za afya, wameendelea kupatiwa huduma hizo kwa utaratibu wa msamaha, hata hivyo, ni kweli kuna changamoto kwenye baadhi ya maeneo atawasilisha"**

# Matukio mbalimbali ya uzinduzi Mbio za Mwenge Moshi jana











# Samia kuzitoa kifungoni Bureau de Change nchini

- Ni zile zilizofungiwa miaka 8 iliyopita
- Fedha na mali kurejeshewa wahusika


Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imepanga muda wowote kuyafungulia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyofungiwa miaka minane iliyopita kwa tuhuma mbalimbali.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema Bungeni jijini Dodoma jana kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, haipo tayari kuona rasilimali na fedha za mtu yeyote zilizochukuliwa, zimebaki serikalini.

Alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Chumbuni, Ussi Salum Pondeza, aliyehoji sababu zilizosababisha maduka ya kubadilisha fedha kuondolewa katika biashara na wananchi wengi kupoteza ajira zao.

Alisema serikali ipo mbioni kufungulia maduka ya kubadilisha fedha nchini ambayo yalifungiwa mwaka 2016 kutokana na tuhuma za utakatishaji fedha, huku wabunge wakitaka maduka yasiyo na hatia yalipwe fidia.

"Serikali itayafungulia maduka hayo muda wowote kuanzia sasa (jana) na kurudishiwa mali na fedha zao zote zilizopokwa na serikali katika operesheni iliyofanyika mwaka 2016.

"Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Ussi wale wote ambao maduka yao hayana makosa, watarejeshewa fedha zao na mali zao, lakini nimpe taarifa tu mwaka ule maduka 68 ndiyo yalifungwa, tayari tumeshafungulia maduka 61, yaliyobaki ni saba na yatafunguliwa muda wowote," alisema.

Alisema serikali ilichukua uamuzi wa kufungia maduka ya kubadilisha fedha mwaka 2016, baada ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kufanya ukaguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na kugundua miamala mbalimbali kwa baadhi ya maduka, kinyume cha matakwa ya sheria na kanuni za usimamizi wa maduka ya fedha za kigeni.

Pia alisema BoT ilifanya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu.

Alisema kufuatia hali hiyo, mwaka 2018 na 2019, BoT kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali, ilifanya operesheni ya ukaguzi maalum kwenye maduka yote ya kubadilisha fedha za kigeni nchini na kubaini makosa mbalimbali, ikiwemo kutofanya utambuzi wa wateja kabla ya kutoa huduma kinyume cha kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu, Sura 423 na kanuni ya 17 ya Kanuni za Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu;

"Kugawa miamala ya wateja kwa lengo la kukwepa kutunza kumbukumbu muhimu zinazoonesha uhalali wa miamala kinyume cha Kanuni ya 23(4) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya mwaka 2015 na kutokutoa stakabadhi za miamala kinyume cha Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya mwaka 2015," alifafanua.

Alisema maduka ya kubadilisha fedha, yalikuwa hayawasilishi taarifa sahihi za miamala BoT na hivyo kuathiri upatikanaji wa takwimu muhimu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi; na baadhi ya maduka yalikuwa yanajihusisha na uhamishaji wa fedha nje ya nchi bila kuwa na leseni wala kibali cha BoT.

**UZINDUZI MBIO ZA MWENGE 2024:**

# Mafanikio makubwa miaka mitatu ya Samia - Majaliwa



**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Watanzania wameshuhudia mafanikio makubwa katika utekelezaji wa dhamira yake ya kuwaletea maendeleo.

Aliyasema hayo akiwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024, sherehe zilizofanyika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro jana.

"Tumeshuhudia mafanikio makubwa ya uongozi wa kiongozi wetu Rais Dk. Samia, tumeona dhamira yake yeye pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika kuwaletea wananchi huduma bora za afya, elimu, maji safi na salama," alisema na kuongeza:

"Pia ameongeza tija katika kilimo, utalii na kuimarisha sekta ya viwanda na kuweka mazingira bora ya uwekezaji."

Kauli mbiu ya Mbio za Mwenge mwaka huu ni: `Tunza mazingira na shiriki chaguzi za Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu.'

Akizungumzia kauli mbiu hiyo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema imetoa wito kwa Watanzania kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao mchakato wake umeshaanza.

Aidha, alisema inawakumbusha Watanzania wenye sifa ya kuchagua na kuchaguliwa, kushiriki uchaguzi huo utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

"...na inatukumbusha wananchi wote kutumia fursa ya kuchagua viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa kote nchini, zoezi litakalokwenda sambamba na wajumbe wa halmashauri kuu za vijiji," alisema na kuongeza, "viongozi hao kwetu sisi ni muhimu sana."

Pia alisema kauli mbiu hiyo inaweka msisitizo kwa jamii nzima kushiriki kikamilifu kaitka uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Hii inatokana na ukweli kwamba suala la utunzaji wa mazingira linamhusu kila mmoja wetu na inatukumbusha wajibu wetu wa kuhakikisha dunia inakuwa mahali salama," alisema.

Alisema sambamba na kauli mbiu hiyo, Mbio za Mwenge mwaka huu, zitaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa lishe bora, mapambano dhidi ya rushwa, Ukimwi na matumizi ya dawa rasmi.

# Askofu David Mwasota aandika historia

## ● Atoa nishani kwa Wachungaji

## ● Apewa Tuzo ya heshima



Askofu Mkuu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly, Dk. David Mwasota akimvalisha medali, Mchungaji Boniface Kamwela (kulia), wa Kanisa la Naioth Mwananyamala juzi Jumatatu ya Pasaka.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly, Dk. David Mwasota akikabidhiwa Tuzo ya heshima kwa uongozi bora kutoka kwa Mchungaji Gideon Lukwaya (kushoto), ambaye ni Askofu Naioth Jimbo la Dar es Salaam juzi Jumatatu ya Pasaka.

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly Tanzania, Dk. David Mwasota, amewashangaza wengi hususan washirika (waumini) wa kanisa hilo baada ya kuamua kuwapa medali za dhahabu Wachungaji wote wa kanisa hilo Jimbo la Dar es Salaam.

Tukio hilo la aina yake, lilifanywa wakati wa Ibada maalum ya Jumatatu ya Pasaka ambapo washirika wa makanisa yote ya Naioth Gospel Assembly Jimbo la Dar es Salaam, walikutana na kufanya ibada moja.

Ibada hiyo ilifanyika Makao Makuu ya kanisa hilo eneo la External jijini Dar es Salaam. Akizungumza kabla ya kuwavalisha medali kama nishani ya heshima kuenzi utumishi wao ndani ya kanisa hilo, Askofu Mwasota alisema akiwa Askofu Mkuu, anaheshimu utendaji wa Wachungaji chini yake.

“Wachungaji hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa yenye mapito na majaribu mengi na ndiyo maana kwa dhati, nimeamua kuwapa medali kuonesha nathamini sana kazi wanayoifanya,” alisema.

Baada ya tukio hilo, Askofu wa Jimbo la Dar es Salaam, Mchungaji Gideon Lukwaya Rashid, akiwakilisha wachungaji wengine, alimshukuru Askofu Mwasota kwa kuwapa heshima hiyo na kueleza kuwa ni la kihistoria kwani halijazoeleka na halijafanywa mahali pengine zaidi ya wao kuona Mkuu wa Nchi, akiwapa nishani kama hizo makamanda wake hususan kwenye Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

“Tukio hili limetupa heshima, hamasa na motisha kubwa. Hivyo tunakuhakikishia Baba Askofu kuwa kazi hii itaendelea kwa viwango ambavyo havijawahi kuonekana kabla,” alisema Askofu wa Jimbo.

Kadhalika, tukio hilo pia liliwagusa waumini wa kanisa hilo na kufurahi kuona wachungaji wao wakiheshimiwa na kiongozi wao mkuu.

Waumini hao walitoa hisia zao kwa shangwe kubwa walioionesha wakati Askofu Mwasota akiwapa wachungaji wao nishani za heshima. Kwa nyakati tofauti, gazeti la UELEKEO liliwasikia waumini wakielezea kuwa Askofu Mwasota, amefanya jambo lili lobeba hisia kuwaheshimu na kwa namna moja au nyingine, ni kama anawashukuru watumishi wa Mungu wanaofanya kazi pamoja naye.

“Mara nyingi wakubwa (Maaskofu), kazi yao ni kupokea tu heshima bila kujali kabisa watenda kazi walio chini yao. Heshima na sifa wanapewa wao tu viongozi wa juu kana kwamba ndiyo wanaofanya kila kitu, lakini leo (juzi Jumatatu), Askofu Mwasota ameonesha tukio la kipekee kuonesha kuwa anafanya kazi na wachungaji, ndiyo maana kanisa hilo sasa linakua kwa kasi,” akisikika mmoja wa waumini akisema.

Wachungaji waliopewa medali za dhahabu ikiwa ni ishara ya nishani ya heshima ni Gideon Lukwaya, Anderson Chogo, Erasto Haule, Festo Kalengela, Boniface Kamwela na Mary Kisinda.

Wengine ni Mary Chacha, Moses Mwakalambile, Bernadeta Mbedule, Floriance Ngaile, Raphael Mwakasege, Frank Mwambete, Tabia Luvanda, Seraphine Gaitani, David Kabika na Rahel Mwasota

Kwa upande mwingine, uongozi wa Jimbo la Dar es Salaam, umempa Askofu wao Mkuu, David Mwasota, Tuzo maalum ya heshima kuenzi na kuthamini kazi kubwa na uongozi wake bora.

Akimkabidhi Tuzo hiyo kwa niaba ya Wachungaji wa Jimbo la Dar es Salaam, Askofu wa Jimbo la Dar es Salaam, Mchungaji Lukwaya, alisema Askofu Mwasota amekuwa kiongozi bora, baba, mshauri na mwalimu mzuri.

“Siku zote ameyafanya haya kwa upendo mkubwa na ushirika bila kuchoka na bila kujali nafasi yake kubwa,” alisema.

# Tanroads yaweka vivuko maalum barabara ya Mwendokasi

**Na Mwandishi Wetu**



WAKALA wa Barabara Nchini (TANROADS) umeweka mazingira mazuri kwa watembea kwa miguu kwenye barabara ya Mabasi ya Yaendayo Haraka (BRT - 3) ya Nyerere jijini Dar es Salaam.

Akizungumza hivi karibuni msimamizi wa mradi huo Mhandisi Frank Mbilinyi, alisema wananchi waendao kwa miguu wanaotumia barabara hiyo, watalindwa kwa kuwekewa, alama za pundamilia na vivuko maalum.

Pia alisema wataweka taa za kuwaruhusu kuvuka kila wanapovuka upande mmoja kwenda mwingine na kutawekwa matuta kwenye barabara ya lami ya kawaida ili kupunguza mwendokasi wa magari.

“Kama mnavyoona kuna taa za kuvukia watu kwenye eneo la kuvukia wananchi hata katika kila barabara za kawaida na zile zenye miundombinu ya mwendokasi kwa kuwasaidia kufika vema wanapokwenda kwenye vituo vya mabasi hayo au kuvuka kutoka upande mmoja na kwenda mwingine,” alisema.

Alisema hawataweza kupata madhara aidha kugongwa na magari au pikipiki, pia kutajengwa vivuko maalum vya wao kupita wanapokwenda kuepusha madhara,” alisema.

Alisema ujenzi huo wa barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT 3) unaotarajiwa kukamilika Machi mwaka huu, umefikia asilimia 45 kwa mkandarasi kuanza kujengea nguzo za vituo vya mabasi, pia kumwagia maji mara kwa mara, ili kuondoa vumbi lisilete madhara kwa watumiaji wa barabara ambayo ujenzi unaendelea.

Mhandisi Mbilinyi alisema barabara za Mabasi Yaendayo Haraka zimeshaanza kujengwa kwa matabaka mbalimbali yakiwemo tabaka la zege kuziruhusu kupitika kwa urahisi.

Aliwata watumiaji wa barabara hiyo wenye vyombo vya moto kuhakikisha wanafuata sheria za barabarani ili kuepuka kusababisha msongamano usio wa lazima.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


HII NI KERO

## Lugha chafu ndani ya mabasi ya umma

KUNA baadhi ya watu wana tabia ya kuporomosha matusi wakiwa ndani ya mabasi pasipo kujali kuwa kuna watoto na watu wa rika na jinsia tofauti. Watu hao huporomosha matusi hayo wakiwa ama wamelewa pombe au kitu kingine cha kilevi. Ukiwaangalia, ni watu wazima tena hapana shaka wana familia majumbani kwao.

Haipendezi na si ustaarabu kufanya hivyo, kwani hiyo ni kero kubwa kwa abiria wenzako. Nawasihi wanaofanya hivyo, wabadilike.





MAONI YA MHARIRI

## Hatua ya kufungulia maduka ya fedha ni ya kupongezwa

Ni jambo jema kusikia kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imepanga muda wowote kuyafungulia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyofungiwa miaka minane iliyopita.

Hayo yalidhihirika jana Bungeni jijini Dodoma wakati Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alipokuwa akijibu swali.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, haipo tayari kuona rasilimali na fedha za mtu yeyote zilizochukuliwa, zinabaki serikalini.

Mapema Mbunge wa Chumbuni, Ussi Salum Pondeza, alitaka kujua ni nini kilisababisha maduka ya kubadilisha fedha kuondolewa katika biashara na wananchi wengi kupoteza ajira zao.

Katika jibu lake, Chande alisema serikali ipo mbioni kufungulia maduka ya kubadilisha fedha nchini ambayo yalifungiwa mwaka 2016 kutokana na tuhuma mbalimbali.

Alisema serikali itayafungulia maduka hayo muda wowote kuanzia jana na wahusika kurudishiwa mali na fedha zao zote zilizopokwa na serikali katika operesheni iliyofanyika mwaka 2016.

Alitaja idadi ya maduka yaliyofungwa kuwa ni 68 na kwamba tayari maduka 61, yameshafunguliwa na kubakia saba ambayo pia yatafunguliwa muda wowote.

Tunaunga mkono hatua hii kwa sababu kurudi kwa maduka hayo, mbali na kusogeza huduma karibu na wananchi, yatasaidia kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Kwa kuwa waswahili wanasema mtego wa panya hukamata waliomo na wasiomo, taarifa ya Naibu Waziri inaonesha kwamba kuna fedha na mali zilikamatwa na vyombo vya dola lakini kimsingi bado ni haki ya wananchi husika ambazo walizipata kwa jasho lao.

Hii imezidi kuonesha namna Rais Samia alivyo mwadilifu mcha-Mungu na anayetembea katika falsafa yake ya R4, yaani maridhiano, kuvumiliana, mageuzi au mabadiliko na kujenga nchi upya.

Hata hivyo, ni imani yetu kwamba haya maduka yatafuata sheria na kanuni za usimamizi wa maduka ya fedha za kigeni na hayatajihusisha na utakatishaji fedha wala kufanya miamala isiyokubalika.

Kwamba sasa maduka haya yatafanya utambuzi wa wateja kabla ya kutoa huduma kama inavyotakiwa na kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu, Sura 423 na kanuni ya 17 ya Kanuni za Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu.

Mbali na taratibu na kanuni nyingine kama zilivyoorodheshwa na Naibu Waziri katika jibu lake ambazo maduka haya yanapaswa kufuata, pia tunaamini sasa yatakuwa yanawasilishi taarifa sahihi za miamala yao BoT na hivyo kusaidia upatikanaji wa takwimu muhimu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

Pia tunaamini itakuwa mwiko kwa maduka haya kujihusisha na uhamishaji wa fedha kwenda nje ya nchi labda kama yatakuwa na leseni au kibali cha Benki Kuu.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


JICHO LANGU

## Tushirikiane kukomesha bangi, mirungi

JANA, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alizindua Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2024 katika Uwanja wa Michezo wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), mkoani Kilimanjaro.

Waziri Mkuu, aliorodesha manufaa ya Mbio za Mwenge ikiwa ni pamoja na kuchochea na kuhamashisha tunu za taifa ambazo ni amani, uzalendo, umoja na mshikamano ndani ya Taifa na pia kuchochea shughuli za maendeleo.

Akasema Mwenge wa Uhuru umekua chombo muhimu katika kuhamasisha uzalendo na pia kuhamasisha jamii ya Watanzania kuhusu lishe bora, kujikinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, ugonjwa wa malaria, mapambano dhidi ya rushwa pamoja na dawa za kulevya.

> **Mwenge wa Uhuru umekua chombo muhimu katika kuhamasisha uzalendo na pia kuhamasisha jamii ya Watanzania kuhusu lishe bora, kujikinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, ugonjwa wa malaria, mapambano dhidi ya rushwa pamoja na dawa za kulevya.**

Hata hivyo, Waziri Mkuu alisema mbio hizo zitaendelea kutoa hamasa kwa jamii kusitisha biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Alikiri kwamba bangi na mirungi zimeendelea kutumika kwa wingi na vijana. Alifafanua kwamba vijana wamekuwa wakitumia aina nyingine ya bangi yenye kiasi kikubwa cha kilevi inayofahamika kwa majina ya "Cha Arusha" na "Skanka". Alitoa wito kwa vijana kuacha kutumia dawa hizo za kulevya akisema dawa hizo, Cha Arusha na Skanka zinawafanya kuwa vichaa.

Aidha Majaliwa alisema Mbio za Mwenge mwaka huu zitaendelea kutoa hamasa kwa jamii kusitisha kilimo haramu cha bangi na mirungi pamoja na kusitisha biashara na matumizi ya madawa ya kulevya.

Ni katika muktadha huo alitoa rai kwa mikoa na wakulima wanaojishughulisha na shughuli za kilimo cha bangi kucha mara moja kwani watakapogunduliwa na kukamatwa hatua kali zitachuliwa dhidi yao.

Kwa kweli, ni vyema wananchi tusaidiane na serikali kunusuru vijana wetu na matumizi ya dawa za kulevya, hususani bangi na mirungi kwani zimekuwa na athari nyingi hasi dhidi yao.

Bila shaka wakulima, wauzaji na hata watumiaji wa hizi dawa tunaishi nao mitaani na vijijini na hivyo ni muhimu kila mmoja wetu asisite kuvijulisha vyombo vya sheria kila anapogundua uwepo wa watu wanaojihusisha na kilimo au biashara ya bangi na mirungi. Hii pia ni pamoja na dawa zote za kulevya ikiwemo kokeni, heroin na nyinginezo pamoja na pombe haramu ya gongo.

Tunaponusuru vijana wetu ambao wanahitajika sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa tunakuwa pia tumeokoa taifa. Shime Watanzania, vita dhidi ya dawa za kulevya ni yetu sote, si ya vyombo vya dola pekee.

# Mafuta yenye afya kwa kupikia






MAFUTA yote yamejaa mafuta na kalori, lakini muundo wake wa kemikali na madhara ya afya, yanaweza kuwa tofauti kabisa.

Mafuta ya kupikia ni chakula muhimu, lakini kuna habari nyingi zinazokinzana kuhusu jinsi uwezo wake wa kiafya.

Kuna aina nyingi za mafuta kutoka ya nazi hadi mizeituni, mboga za kijani hadi kanola, parachichi hadi ufuta .

Mafuta yanayofaa kutumia na yanayopaswa kuepuka

Mafuta ya kupikia kwa kawaida, yana majina yake kama vile ya karanga, mbegu, matunda, mimea au nafaka ambako hutoka ama kwa kuponda, kukandamiza au kusindika.

**MAFUTA YA NAZI**

Katika muongo uliopita, mafuta ya nazi ambayo yana takriban asilimia 90 ya mafuta yaliyojaa, yamekuwa miongoni mwa vyakula bora vya kisasa.

Yamesifiwa kuwa chakula cha hali ya juu (miongoni mwa mambo mengine, kwa sababu kuna uwezekano mdogo wa kuhifadhiwa mwilini kama mafuta na kuna uwezekano mkubwa wa kutumiwa kama nishati), lakini mtaalamu wa magonjwa wa Chuo Kikuu cha Harvard anasema ni `sumu mwilini.'

Kutumia mafuta yaliyojaa zaidi ya gram 20 kwa wanawake na gram 30 kwa wanaume kwa siku, kulingana na miongozo ya Uingereza, husababisha mwili





kuzalisha cholesterol mwilini, ambayo huongeza hatari ya ugonjwa wa moyo.

**Zipo aina tatu za asidi ya mafuta:**

Mnyororo mfupi, wa kati na mrefu. Asidi ya mafuta ya mnyororo mfupi na wa kati, hufyonzwa ndani ya damu na kutumika kama chanzo cha nishati, lakini asidi ya mafuta ya mnyororo mrefu, husafirishwa hadi kwenye ini, na hivyo kuongeza viwango vya cholesterol katika damu.

"Mafuta ya nazi yalikuwa maarufu miaka kadhaa iliyopita yalipodaiwa kuwa na athari maalum," anasema Alice Lichtenstein, Profesa wa Sayansi ya Lishe na Sera katika Chuo Kikuu cha Tufts, Massachusetts.

"Lakini ukiangalia tafiti zinazolinganisha mafuta hayo na mengine, matokeo yanaonesha kuwa ina mafuta mengi yaliyojaa na hakuna majaribio ya kliniki yanayounga mkono madai hayo ya awali."

Uchunguzi unaonyesha kuwa mafuta ya nazi yana mafuta mengi.

Majaribio mengi yaliyodhibitiwa bila mpangilio maalum, yanaonesha kuwa mafuta ya nazi huongeza viwango vya cholesterol hatari, lipoprotein ya chini (LDL), ambayo inahusishwa na ugonjwa wa moyo na kiharusi, lakini pia huongeza cholesterol yenye faida, HDL, ambayo huondoa LDL kutoka mkondo wa damu.

Mapitio ya 2023 ya majaribio yaliyodhibitiwa bila mpangilio, yalihitimisha kuwa mafuta ya nazi yana athari kidogo kwa LDL kuliko siagi, lakini siyo mafuta ya alizeti.

Chkaula kilichojaa mafuta mengi kinaweza kuongeza cholesterol ya HDL kwa sababu kina kiasi kikubwa cha asidi ya lauriki, ambayo imegunduliwa kuongeza viwango vya juu vya protini HDL katika damu zaidi ya viwango vya chini vya protini au LDL.

Lakini Taylor Wallace, Profesa Mshiriki Idara ya Lishe na Mafunzo ya Chakula katika Chuo Kikuu cha George Mason huko Virginia, anashikilia kuwa asidi ya lauric haina afya bora kama wengine wanavyodai.

Imeelezwa kama asidi ya mafuta ya C12, kumaanisha kuwa ina atomi 12 za kaboni na hiyo inaiweka kwenye ufafanuzi wa asidi ya mafuta ya mnyororo wa kati.

"C12 ni kama asidi ya mafuta ya mnyororo mrefu ambayo imeainishwa kama mnyororo wa kati," anaelezea Wallace. "Takriban asilimia 70 ya C12 huonekana kama asidi ya mafuta ambayo husafirishwa hadi kwenye ini."

Asidi za mafuta ya mlolongo mrefu, ina uwezekano mkubwa wa kuhifadhiwa kwenye ini kama mafuta na baada ya muda, zinaweza kusababisha matatizo ya afya kama vile ugonjwa wa ini ambalo halijaathiriwa na ulevi.

Badala yake, wataalam wanashauri kuchagua mafuta yenye uzito wa kiwango cha chini huku yakiwa ni kiwango cha juu cha mafuta mengine yenye afya.

Imethibitishwa kuwa mafuta ya polyunsaturated (omega 3 na omega 6) na mafuta ya

>>>Inaendelea Uk. 8

# Mafuta yenye afya kwa kupikia

>>>Inatoka Uk. 7

monounsaturated, hupunguza cholesterol na kutoa asidi muhimu ya mafuta na vitamini.

Hupatikana katika aina nyingi tofauti za mafuta ya mboga, ingawa kiasi halisi kinategemea mmea na mchakato wa kiteknolojia unaotumiwa wakati wa uzalishaji.

Wataalamu wanashauri kuchagua mafuta yenye kiwango cha chini cha mafuta na kiwango cha juu ya aina ya mafuta mengine yenye afya kwa kiasi.

"Tafiti nyingi zinaonesha kuwa vyakula vilivyo na mafuta mengi ya monounsaturated na polyunsaturated, vinahusishwa na hatari ndogo ya ugonjwa wa moyo na mishipa," Lichtenstein anasema. "Inapendekezwa kuchukua nafasi ya vyanzo vya mafuta yasiyosafishwa na mafuta ya polyunsaturated, hasa mafuta ya mboga, karanga na mbegu," anaongeza.

Utafiti ulihusisha kuchukua nafasi ya mafuta yaliyojaa na kubadilisha na mafuta ya zeituni, kwa mfano, ambayo yana hatari ndogo ya kusababisha ugonjwa wa moyo. Kubadilisha siagi, majarini, mayonesi au mafuta ya maziwa kwa mafuta ya mizeituni kunapunguza hatari kwa asilimia tano hadi asilimia saba.









Uchambuzi wa 2021 wa idadi ya watu ambao uliolinganisha afya ya watu na matumizi yao ya siagi, majarini, mafuta ya mahindi, mafuta ya canola na mafuta ya mizeituni kwa zaidi ya miaka 15, uligundua kuwa, kwa ujumla, kupika kwa mafuta ni afya kuliko kutumia siagi na majarini.

**MAFUTA YA MIZEITUNI**

Marta Guasch-Ferre, Mwandishi na Mwanasayansi wa Utafiti katika Idara ya Lishe katika Shule ya Afya ya Umma ya TH Chan katika Chuo Kikuu cha Harvard huko Boston, alichambua afya na lishe ya zaidi ya watu 100,000 kwa zaidi ya miaka 24 na kugundua kuwa wale waliotumia mafuta ya mzeituni walikuwa na hatari ya chini ya asilimia 15 ya ugonjwa wa moyo.

Faida za kiafya za mafuta ya mzeituni zinaweza kuhusishwa kwa sehemu na asidi yake ya mafuta ya monounsaturated, ambayo yana vitamini na madini na polyphenols na virutubisho vodogo vinavyotokana na mimea.

"Lakini siyo tu juu ya kuongeza mafuta ya mzeituni kwenye lishe, ni juu ya mafuta ya mizeituni kuchukua nafasi ya mafuta mengine ambayo hayana afya," anasema Guasch-Ferre.

Mafuta ya mizeituni, ambayo hupatikana kwa kusaga mizeituni na kutenganisha mafuta kutoka kwa massa yao, yanajulikana kuwa mafuta ya afya zaidi ya mboga. Utafiti uligundua kuwa mafuta ya mizeituni yanaweza kuwa na faida katika kuzuia ugonjwa wa moyo na kisukari cha aina ya mbili.

Uchunguzi wa 2023 wa tafiti ulipata ushahidi kwamba mafuta ya mizeituni yanaweza pia kuboresha hatari ya kupata magonjwa ya mfumo wa neva kama vile Alzheimer's na yanaweza kusaidia na dalili za wasiwasi na unyogovu,na vilevile yanaweza kusababisha mabadiliko katika microbiome ya utumbo.

**MAFUTA YA PARACHICHI**



Mafuta ya parachichi - ambayo ni mgeni katika soko la mafuta, yana kiasi kikubwa cha phytochemicals na asidi oleic na yanaweza kupatikana kutoka kwa matunda sawa na mafuta ya mzeituni ambayo huhifadhi zaidi kemikali za afya zinazopatikana kwenye mmea.

Watafiti wanasema katika nakala yao ya 2019 kwamba, kulingana na joto ambalo mafuta hayo yanahifadhiwa na kwa muda gani, mafuta ya parachichi yanaweza kuchukuliwa kuwa mbadala mzuri wa mafuta ya mizeituni, kwa sehemu kutokana na maudhui yake ya antioxidant na phenol. Mafuta haya ni sawa na yale ya mzeituini.

Katika utafiti mmoja, watu 13 walikunywa kifungua kinywa chenye mafuta mengi kilicho na siagi ya parachichi au mafuta. Watafiti kisha walichambua damu yao na kugundua kuwa wale waliotumia mafuta, walilindwa zaidi dhidi ya athari za kifungua kinywa cha mafuta.

- Imani potofu kuhusu jinsi ya kupunguza mafuta mwilini
- Faida tano za kula samaki wenye mafuta

**MAFUTA YA UFUTA**

Mafuta ya ufuta hupatikana kutoka kwa mbegu za ufuta zilizochomwa au mbichi, zilizojaa vitamini, madini, protini na nyuzi.

Uchunguzi wa 2020 wa tafiti kuhusu madhara ya mafuta ya ufuta kwa afya yetu ulihitimisha kuwa kuna ushahidi fulani wa kupendekeza kwamba inaweza kuboresha alama fulani za viumbe (viwango katika damu vinavyoonyesha hatari ya kupata magonjwa fulani).

Hata hivyo, ushahidi ni mdogo na tafiti zaidi zinahitajika.

**MAFUTA YA KANOLA**

Mafuta ya Canola, yanayotokana na ua la manjano lenya jina kama hilo, yana viwango vya chini vya mafuta yaliyojaa mafuta na viwango vya juu vya mafuta ya monounsaturated na polyunsaturated, ikiwa ni pamoja na asidi ya oleic.

Uchunguzi wa tafiti kuhusu faida za kiafya za mafuta ya canola ulihitimisha kuwa yanaweza kusaidia kupunguza kolesteroli na hatari ya kupata kisukari cha aina ya 2, ikilinganishwa na vyakula vingine vyenye mafuta mengi. Kwa ujumla, inaweza kuwa nyongeza nzuri kwa lishe.

Hata hivyo, mwaka 2017, wanasayansi walilisha panya lishe iliyojaa mafuta ya canola na wakahitimisha kuwa waliongeza uzito zaidi kuliko panya ambao waliendelea na lishe isiyo na mafuta hayo.

BBC.

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo
JARIDA
Jungu Kuu
| Jumatano April 3 - 9, 2024 |

JAMII
UCHUMI
SIASA

Jarida hili haliuzwi

# Wapinzani: ndani wanasigina demokrasia, nje wanaidai!



UK. 12 & 13

# Vijana wa kiume amkeni, msibweteke, msidanganyike

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Hakuna aliye kama Mungu wetu aliye hai na mwenye kuturehemu kila kukicha. Anatupenda na kututakia mema wote wenye mwili na hukumu zake ni za haki, hivyo inatupasa kumcha Yeye na kumshukuru pasipo kuchoka.

Sehemu ya kwanza ya makala hii ilimalizia kwa kuwaomba viongozi wa taifa letu walio na dhamana ya kutuongoza wasifumbienmacho maovu kama ya ushoga na usagaji bali wasimame katika kweli na hiyo na kwa hakika kweli itatuweka huru na salama mbele za Mwenyezi Mungu. La sivyo taifa litaadhibiwa kwa kuukumbatia 'uovu'.

Pamoja na angalizo hilo kitaifa, vijana wa kiume wajiulize nini kimejiri hadi kujiona wanyonge kiasi cha kutopenda kuoa na kuwa 'baba' wa familia?

Maelezo ninayoyapata toka kwa baadhi yao hayatoshelezi hata kidogo. Kusema hali ya maisha imekuwa ngumu siyo utetezi bali vijana mnajiweka kwenye sintofahamu kwa matakwa yenu wenyewe maana mnakiuka kanuni ya 'urithi' wetu.

Imeamndikwa 'utawaacha wazazi wako nawe utaambatana na mkeo na wawili mtakuwa mwili mmoja'. Mkiishi pamoja kwa kupendana huku mkikabiliana na mema au mabaya mwisho mtafanikiwa.

Hii inamaanisha kujizatiti kwelikweli ili kukabiliana na lolote litakalotokea mkiwa mume na mke huku mwanaume akimtia moyo mkewe kwa kupambana bila kuchoka.

Tangu enzi za mababu zetu hadi sasa maisha yamekuwa siyo 'lelemama'; ni pamoja na kupambana na mazingira yaliyo mbele yetu kwa faida yetu na watoto watakaozaliwa kupitia. 'taasisi ya ndoa'.

Sasa kizazi hiki kinaiharibu misingi ya familia kutokana na vijana wanaotakiwa kuwa 'baba' wa familia, lakini wanajiona wanyonge hivyo kujikita zaidi kwenye 'maovu' na kujenga tabia zisizofaa katika jamii.

Tuseme nini juu ya hali hiyo isiyofaa kwa vijana wetu, hasa wa kiume kudharau wajibu wao waliopewa tangu kuumbwa kwa binadamu? Tumwombe Mungu kupitia toba ya kweli na kuomboleza ili nguvu ya kimbingu irehemu vijana wetu na wabadirike kimtazamo na kifikra na kurejea kwenye uhaliasia wao wa kuoa na kuitunza familia.

Kwa bahati mbaya, mabinti/ wasichana baadhi yao wanachangamkia 'udhaifu' huo na kupelekea wao kuwa na familia. Kinachojiri sasa wanawake wamekuwa wajasiriamali wazuri na kutokana na mafanikio fedha, wanatafuta/ kununua viwanja, wanajenga nyumba, wananunua magari na kadhalika. Kupitia njia hiyo wanawanasa vijana wa kiuma kirahisi; hatimaye kuishi kama mume na mke (hata bila kujali taratibu zinazotakiwa kufuatwa hadi kufunga ndoa. Sasa anaoa au anayeolewa ni msichana/ mwanamke au kijana wa kiume? Hapa msingi wa kanuni ya ndoa umetetereka: vijana wa kiume kulikoni?

Tuache utani! hali hiyo haipendezi hata kidogo kijana mtanashati unatekwa kirahisi kwa kisingizio cha maisha kuwa magumu. Kwa nini usijiulize huyu anayeniteka, amefanyaje mpaka akafikia hali ya kunivuta bila ya kujitetea?

Hakuna namna vijana wetu wa kiume rudini kwenye 'reli' na muweze kuendesha garimoshi' bila kutetereka, la sivyo kuna kukwama mbeleni kutokana na kutojitambua sawasawa.

Mnatakiwa kuwa na malengo yenye tija na kuufahamu wajibu wenu kwamba 'mke' unayemuoa anatoka kwao anakuja kwako siyo wewe kutoka kwenu na kuhamia kwake. Kufanya hivyo ni kukiuka maadili mema na kupoteza heshima ya kiume.

Zitafakarini njia zenu na mrejee kwenye misingi ya ndoa iliyowekwa tangu enzi za 'Adam' na 'Hawa'. Hata wakati huo Adam hakwenda kwa Hawa bali Hawa ndiye aliyeletwa kwa Adam ikiashiria msichana kuachana na wazazi wake na kuambatana na mumewe na kuwa kitu kimoja.

Ilikuwa ndoa ya kwanza iliyofungwa na Mungu mwenyewe ingawa suala la 'mahari' wakati huo halikuwepo bali Mungu alitaka kuanzisha 'taasisi ya ndoa' na mengine (kama mahari) yatafuata lakini kwa utaratibu na misingi inayokubalika kijamii na kiroho pia.

Sasa kinachotakiwa ni vijana wetu kuwa makini katika kutunza na kuimarisha heshima yao ya kuitwa 'mwanamume bora' mwenye kuipenda na kuitunza familia yake. Tuondokane na 'roho' za kuwa tegenezi au kupenda maisha rahisi hadi kupelekea kujidhalilisha pasipo sababu za msingi.

Uliumbwa uwe mwanamume hivyo kaza buti, songambele kama askari vitani akitetea taifa yake.

Vivyohivyo, kijana mwanamume usilegee maana kufanikiwa kimaisha ni kuwa na mtazamo chanya ikiwa ni-pamoja na "Kumcha Mwenyezi Mungu" na "Kumwabudu" katika roho na kweli. Ukifanya hivyo hutakosa Rehema za Mungu na atakujalia kupitia maarifa ya kimbingu uweze kumpata mke mwema kwa kuzingatia maandiko kuwa: "mke mwema" hutoka kwa Mungu na hatimaye atakuwezesha kuwa mume hodari wa vita kuilinda familia yako.

Kwa kuwa misingi za kuwawezesha vijana kuwa wanaume thabiti zinapindishwa kwa manufaa binafsi; kiasi kwamba wasichana na wanawake wanachukua fursa na kujizatiti na hivyo kuwazidi kete vijana wakiume. Vilevile, suala la kuwaacha wazazi na kuambatana na mkewe na kuwa kitu kimoja linawayawaya; hivyo misingi ya kuyamudu maisha ya kifamilia imeharibika.

Huko nyuma wazazi wetu walikuwa nguzo muhimu katika kujenga uimara kwa familia za watoto wao wa kiume. Upendo ulitawala na vijana wakitii sauti za wazazi na kutambua kuwa harakati zao (wazazi) zinalenga kuwatakia maisha mema na yenye baraka tele.

Kusudi la makala hii siyo kulaumu bali ni kujenga uwelewa kwa vijana wetu kwamba lazima kijana mwanamume ajivunie kuwa baba mwenye familia yake.

Katika tamaduni na mila za kiafrika, kijana ndiye mwendelezaji wa 'ukoo'. Yawezekana yapo makabila machache ambayo msingi wa ukoo umewekwa kwa mwanamke au mjomba lakini kimsingi ni kwa wanaume mwenye kurithi na kuendeleza ukoo husika. Lakini tuseme nini maana misingi ikiharibika mwenye haki atafanyaje?

Hata hivyo, nyakati hizi zinaitwa: 'kizazi cha kidijiti' hivyo masuala ya utandawazi, mitandao ya kijamii kupitia 'simujanja', kompyuta mpakato, vishikwambi, luninga, na kadhalika vimesababisha mageuzi makubwa katika makabila mengi hapa nchini kiasi kwamba misingi ya awali ya kikabila na koo mbalimbali haithaminiwi tena.

Vijana wetu wengi wamezama katika matumizi ya vifaa vya kidijiti hadi kujipatia wake au kuanza mahusiano kupitia mitandao ya kijamii na njia nyinginezo za kidijiti.

Walioanzisha teknolojia hizo wanashabikia kinachoendelea barani Afrika hadi kulazimisha kile wanachouta 'haki za binadamu' kiasi kwamba hata baadhi ya mataifa barani Afrika yatunge sera na sheria zinazoshabikia 'vitendo vya uovu'. Hii maanake nini? Ni dalili za viashiria vyenye kuonesha kuwa "mpinga" Kristo ananyatianyatia.

Mataifa yaliyoendela na ambayo ni chimbuko la elimu ya Kikristo na hatimaye wakaweza kutuletea 'Habari Njema' takribani zaidi ya miaka 100 iliyopita; sasa wanarejea kwenye kusambaza 'uovu' kupitia kisingizio cha "haki za binadamu".

Hizo ni haki gani kwa mwanaume kufunga ndoa na mwanauume mwenzake? Kama siyo makusudi ya kupingana na mapenzi ya Mungu tunayemwabudu na kumtegemea kwa maisha yetu ya kila siku wakati ni uovu uliokithiri? Inasikitisha sana.

Tunahitaji hekima ya kimbingu itusaidie ili tutambue yaliyo chukizo mbele za Mungu tusiyakumbatie. Nakubali, tumo kwenye ulimwengu wa kidijiti lakini kisiwe kisingizio cha kudhalilisha utu wetu na kufanya mambo ambayo hata wanyama hawafanyi.

Mungu alituumba kwa sura na mfano wake hivyo tujiheshimu na tutende yaliyo mema na kutendeana haki. Wenye pesa kunyanyasa wasionazo siyo jambo jema hata kidogo.



Sikatai kuwepo haki za binadamu na demokrasia pamoja na uhuru wa mtu kufanya anavyotaka; lakini ikifika mahali kuwepo mipaka kati ya ulimwengu wa kimwili na kiroho.

Mwenyezi Mungu aliyeasili ya mema yote aendelee kuheshimiwa na kuogopwa na kila mwenye mwili. Wakati huohuo, vigezo na masharti husika vikizingatiwa kwa kutii na kunyenyekea mbele yake Mungu. Roho za kuchochea uovu ili ufanyike kupitia 'dirisha' la 'haki za binadamu' pamoja-na teknolojia za kidijitali na/au TEHAMA; zikemewe ipasavyo zisijiinue kwenye ulimwengu wa kimwili.

# Falsafa, dhana na umuhimu wa Mwenge bado uko palepale

Na Mwandishi Wetu

JANA, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2024 katika Uwanja wa Michezo wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), mkoani Kilimanjaro.

Mbio za Mwenge mwaka huu pia zinakwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 60 ya muungano wa nchi yetu na Zanzibar.

Mwenge huo baada ya kuzinduliwa jana ulikabidhiwa kwa vijana sita kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuukimbiza katika mikoa 31 yenye jumla ya halmashauri 195 za Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa siku 195.

Imeelezwa kwamba mbio hizo za Mwenge zitaendelea kuhamasisha amani, umoja, upendo na mshikamano wa kitaifa pamoja na kuwahimiza wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa mwaka huu ni 'Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu.'

Makala hii, pamoja na mambo mengine inalenga kuonesha umuhimu wa Mbio za Mwenge kwani baadhi ya wapinzani wamekuwa wakiponda kuendelea kuwa na mbio za Mewenge.

## HISTORIA YA MWENGE

Historia ya nchi yetu ni pana na ya kuvutia kwa namna ya pekee ukilinganisha na nchi nyingi za Afrika na Duniani kote. Upekee huu unatokana na uwezo wa kujenga hoja na uadilifu wa viongozi wetu, hasa mwasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipochaguliwa kuwa mjumbe kwenye Baraza la kikoloni la kutunga Sheria (Tanganyika Legislative Council) mwaka 1958.

Kwa kuwa Mwalimu alikuwa na ndoto ya kuiona Tanganyika na Afrika iliyo huru, mwaka 1958 katika hotuba yake ya kwanza alitamka maneno ya kifalsafa kwa wajumbe na Spika wa Baraza la kikoloni la kutunga Sheria kwa kusema: "Sisi tunataka Uhuru wa Tanganyika, Mkitupatia tutauwasha Mwenge wa Uhuru na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje na mipaka yetu, ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau."

Maneno haya aliyarudia tena mwaka 1959 alipohutubia kikao cha 35 cha Baraza la Umoja wa Mataifa kama Mbunge mwakilishi pekee wa Tanganyika.

Falsafa hiyo ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilikuwa ni kiashiria kikubwa kwa Waingereza kwamba watu wa Tanganyika wamechoka kutawaliwa.

Siku Tanganyika ilipopata Uhuru Desemba 9, 1961, Mwalimu Nyerere aliuwasha Mwenge wa Uhuru na akamkabidhi Luteni Alexander Nyirenda na kikosi cha vijana wenzake, wakaupeleka Mwenge wa Uhuru juu ya Mlima Kilimanjaro.

Mwalimu wakati akitoa hotuba ya siku ya Uhuru; aliwatangazia Watanganyika, Afrika na Dunia kwa ujumla kwa kusema "Sisi tumekwisha uwasha Mwenge wa Uhuru na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima mahali palipo jaa dharau."

Luteni Alexander Nyirenda akipandisha Bendera na Mwenge wa uhuru juu ya Mlima Kilimanjaro usiku wa kuamkia Desemba 9, 1961.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika na kuwashwa kwa Mwenge wa Uhuru, Mwalimu Nyerere na viongozi wenzake wa awamu ya kwanza walielekeza juhudi zao katika kuwaunganisha Watanzania na kuweka misingi imara ya kulijenga taifa huru la Tanganyika; kudumisha amani, upendo, umoja, mshikamano na kuweka sera za kukabili maadui ujinga, umaskini na maradhi.

Awamu hii ilitafsiri falsafa ya Mwalimu aliyoijenga katika Mwenge wa Uhuru kwa kuweka misingi madhubuti ya uhusiano wa nje, sera ya kutofungamana na siasa za upande wowote, na kuweka msisitizo mkubwa katika ukombozi wa Bara la Afrika na mapambano dhidi ya ubeberu na vibaraka wao.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Azimio la Arusha lililosisitiza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, na kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni matunda ya utelekezaji wa Falsafa ya Mwenge wa Uhuru.

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari mwaka 1964, Tanganyika iliungana na Zanzibar na kupata Taifa moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya ni mafanikio makubwa katika kutekeleza falsafa ya Mwenge wa Uhuru kwani Wazanzibar walirejeshewa matumaini yaliyokuwa yametoweka chini ya utawala wa Kisultani.

Hata baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964, falsafa ya Mwenge wa Uhuru iliendelezwa kwa kuukimbiza Mwenge wa Uhuru katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kujenga na kuimairisha misingi ya amani, umoja, uzalendo, upendo, mshikamano na kuhamasisha shughuli za maendeleo katika jamii zetu na kupeleka kwa Watanzania wote ujumbe maalumu uliokusudiwa na Serikali kila mwaka.

Aidha, Mwenge wa Uhuru ni chombo pekee tulichonacho kama taifa cha kuwaunganisha Watanzania na kuwa wamoja kwani haufungamani na itikadi za kisiasa, makabila yetu wala dini zetu. Mwenge wa Uhuru ni mali ya Watanzania wote.

## MWENGE KUSIMAMIWA NA SERIKALI

Hadi mwaka 1992, Mbio za Mwenge wa Uhuru zilikuwa zikisimamiwa na kuratibiwa na chama tawala kwa maana ya Chama Cha Mapinduzi.

Baada ya nchi yetu kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992; mwaka 1993 Mbio za Mwenge wa Uhuru zilianza kusimamiwa na Serikali chini ya Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Vijana kwa pande zote mbili, Muungani na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mabadiliko hayo yalikuwa ni kiashiria kikubwa kwa Watanzania wote kwamba Mwenge wa Uhuru hauna Chama, hauna kabila na hauna dini isipokuwa ni kwa ajili ya kujenga na kudumisha umoja wa kitaifa.



Tangu Mbio za Mwenge wa Uhuru ziasisiwe hadi leo, misingi na madhumuni ya Mwenge wa Uhuru na Mbio zake zimeendelea kuwa zenye manufaa makubwa na zitaendelea kurithishwa vizazi hadi vizazi katika taifa letu.

## FAIDA ZA KITAIFA, KIMATAIFA

Mwenge wa Uhuru umekuwa ni chombo muhimu cha kujenga undugu, umoja, mshikamano na kudumisha amani pote unapopita bila kujali itikadi zetu za kisiasa, dini wala makabila yetu.

Umuhimu huu unatokana na ukweli kwamba, leo hii tunahitaji kujenga Taifa lenye amani, umoja, upendo na mshikamano wa kitaifa kuliko wakati wowote ule ikiwa ni pamoja na kujenga taifa lisilokuwa na dhuluma, unyonge, rushwa, ubaguzi, ukabila, udini wala vitendo vya kifisadi.

Mbio za Mwenge wa Uhuru zimeendelea kuhamasisha wananchi kwa kushirikiana na Serikali yao katika kubuni na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika nyanja za kilimo, ufugaji, Uvuvi endelevu, uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu, maji, umeme na huduma za jamii katika maeneo yote nchini na hasa katika maeneo yasiyofikika kiurahisi.

Kwa watakaofuatilia Mbio za Mwenge, watasikia miradi mingi sana itakayokuwa inazinduliwa na kukaguliwa na mbio hizo huku fedha zikitokana na serikali na hata nguvu za wananchi.

Hata hivyo, michango mingi inayotolewa na wananchi ni ya hiari mara nyingi hutolewa baada ya wananchi kuhamasishwa na kufahamu umuhimu na matumizi yake ambayo ni kugharamia kwa miradi yao wenyewe.

Mbio za Mwenge wa Uhuru zimekuwa zikitumika kuelimisha wananchi katika maeneo yote nchini jinsi ya kupambana na maradhi yanayotishia ustawi wa watu wetu kama vile Ukimwi, Malaria na kupambana na matumizi ya Dawa za kulevya.

Pamoja na njia nyingine zinazotumika kuwahamasisha wananchi wetu, bado Mbio za Mwenge wa Uhuru zimekuwa ni njia sahihi ya kufikisha taarifa na elimu sahihi ya changomoto hizi kwa watanzania wote.

Mbio za Mwenge wa Uhuru pia, zimeendelea kuhamasisha na kuimarisha umuhimu wa Muungano kwa Watanzania wa pande zote mbili za nchi yetu.

Kimataifa, Mwenge wa Uhuru umeendelea kusimamia dhana ya na maudhui yake ya kumulika hata nje ya mipaka yetu. Kwani umeendelea kuhamasisha amani ndani ya Afrika Mashariki, Kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika na Duniani kwa ujumla.

Tanzania imeendelea kuwa msuluhishi wa Amani Afrika na mfano wa kuigwa kwa mataifa mengine duniani kote na imeshiriki ukombozi wa Bara la Afrika hasa kusini mwa Afrika na kusisitiza juu ya umoja, mshikamano, upendo na amani kwa mataifa hayo.

Mwenge wa uhuru umeendeleza falsafa ya kumulika ndani ya mipaka ya taifa letu kwa kumulika uovu katika jamii ikiwemo uzembe, kutowajibika, vitendo vya rushwa na ufisadi katika miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii nchini.

Mbio za Mwenge wa Uhuru pia hutumika katika kuratibu na kutathimini shughuli mbambali za maendeleo zinazofanywa na wadau wa maendeleo na kukusanya taarifa zinazohusu kero za wananchi ambazo husaidia Serikali katika upangaji na utelezaji wa mipango ya maendeleo kwa wananchi wake.



# Wapinzani: ndani wanasigina demokrasia, nje wanaidai!

**Na Hamid Yassin**

DESEMBA 17 na 18 mwaka 2018 viongozi wa vyama sita vya siasa vya upinzani walikutana mjini Unguja Zanzibar, kwa wito wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) kwa nia ya kujadili hali ya kisiasa hapa nchini.

Vyama vilivyokutana ni CUF, Chadema, NCCR-Mageuzi, NLD, ACT-Wazalendo na Chauma. Nakumbuka miongoni mwa watu waliowakilisha vyama hivyo ni pamoja na Marehemu Seif Sharif Hamad, Freeman Mbowe, marehemu Edward Lowassa, Fredirick Sumaye (kabla hawajarejea CCM), James Mbatia, Mzee Hashim Rungwe, na Zitto Kabwe.

Akiongea na waandishi wa habari baada ya kikao kile cha siku mbili za viongozi hao; aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF; Hayati Maalim Seif Sharrif Hamad alisema viongozi hao walipitisha maazimio kadhaa na ambayo yangekuwa ni agenda kuu kwa mwaka uliofuata, yaani 2019.

Pamoja na mambo mengine; yalitolewa maazimio na au matamko ya kwamba; mwaka 2019 ulikuwa ni mwaka wa kudai demokrasia na haki ya vyama kufanya mikutano ya hadhara na maandamano na pia walipitisha azimio kwamba, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na aliyekuwa Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko waliokuwa wanashikiliwa katika gereza la Segerea jijini Dar es salaam, walikuwa ni wafungwa wa kisiasa!

Kikao chao ambacho hakikuwa kinarushwa moja kwa moja kwenye vyombo vya habari na wala kuhudhuriwa na waandishi wa habari, mambo yangeweza kuishia humo ukumbini ni wazi tusingejua waliyokubaliana mle ndani.

Lakini kwa sababu na kwa hiari yao waliamua kuongea na waandishi wa habari; ni wazi kuwa walitaka umma ujue kilichojiri na pengine walitaka umma uwaunge mkono.

Kupitia vyombo vya habari, umma ulijuzwa kilichowakalisha kitako watu wale, nami ninayo haki yangu ya kuwakumbusha umma wa Watanzania kupitia Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi inayoniruhusu kutoa mawazo na hususani juu ya matamko ya watu kama hawa.

Kazi ya kusoma, kufikiri, kuchambua na kuandika ni kazi ngumu sana. Ni kazi inayohitaji muda, utulivu, uvumilivu na ustaarabu. Ni kazi ngumu, lakini pia ni kazi ya wajibu kwa watu makini.

Kudai demokrasia ni jambo zuri na pia ni jambo la afya kwa ustawi wa taifa letu katika miaka mingi ijayo. Hivyo ile kauli kwamba eti Freeman Mbowe na Esther Matiko walikuwa wafungwa wa kisiasa, katu haikuniingia akilini na wala haikubaliki kwa watu makini kwa sababu hawa walikuwa hawajafungwa. Walikuwa mahabusu na kesi zao zikiendelea.

Inasikitisha kwa viongozi niliowataja hapo juu wakiwemo

watu walowahi kuwa mawaziri wakuu kutoa azimio kuwa waliokuwa mahabusu (Freeman Mbowe na Esther Matiko) kwamba walikuwa wafungwa wa kisiasa.

Leo nimeamua kuongelea umuhimu wa kudai demokrasia tu na wala si juu ya kesi ile iliyowakabili watuhumiwa na mahabusu wale wa Chadema ambayo hata hivyo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan 'wanayemnanga' hivi sasa huko kwenye majukwaa ya maandamano yao aliwafutia zile kesi zao!

Jambo ambalo ninadhani litachukua muda mrefu wa kulizungumzia ni hili la viongozi hawa kudai demokrasia. Pamoja na kwamba; kwa mujibu wa tafsiri ya Kamusi yetu ya Kiswahili neno demokrasia lina maana ya mfumo wa kuendesha serikali iliyochaguliwa na watu kwa manufaa ya watu; lakini maneno 'uhuru wa mawazo' kuwa haki ya binadamu hayawezi kukosekana katika tafsiri yoyote ya maana ya demokrasia.

'Locus stands' ni neno lililozoeleka sana mahakamani, maneno haya yanamaanisha juu ya uhalali wa mtu aliye na tatizo kwenda mahakamani, kama ndiye alistahili kwenda hapo na si mtu mwingine.

Nimeurejea msemo huu wa Kiingereza kwa sababu kikundi cha viongozi waliokutana Zanzibar mwaka ule kwa wito wa Katibu Mkuu wa CUF; hawawezi kufungua midomo yao na kusema wanadai demokrasia.

Ninaamini, azimio la kusema Freeman Mbowe na Esther Matiko kuwa walikuwa ni wafungwa wa kisiasa, kama lingepelekwa kwenye sekretariati za vyama vyao ambavyo vina idara mbalimbali zikiwemo idara za sheria, azimio hilo au lingekataliwa au lingerekebishwa.

### UKARIMU HUANZIA NYUMBANI

Waswahili wana usemi wao kwamba ukarimu huanzia nyumbani. Haiwezekani ukajadili suala la kukosekana ukarimu kwa jirani wakati wewe mwenyewe nyumbani kwako huna ukarimu wowote.

Waungwana pia wanasema kabla hujazungumzia kibanzi kwenye jicho la mwenzako, ondoa kwanza boriti kwenye jicho lako.

Vivyo hivyo hata demokrasia, inatakiwa ianzie ndani ya vyama, na ile ya nje iwe ni kwa ajili ya kuongezea ile iliyomo ndani. Je, kuna demokrasia ndani ya vyama vyetu?

### HALI ILIVYO NDANI YA CHADEMA YA MBOWE

Ukirejea waraka wa mkakati wa mabadiliko ulioandikwa miaka 10 iliyopita (2013) na baadhi ya viongozi wa Chadema, ulionesha dhahiri kwamba uongozi sasa wa chama hicho haruhusu demokrasia wala kubadilishana kijiti cha uongozi.

Katika utangulizi wa waraka huo, wahusika waliandika namna hii: "Taasisi tunayoizungumzia (Chadema) ilisajiliwa rasmi mwezi January 1993 na kutokea wakati huo imeongozwa na wakuu wa taasisi wapatao wawili na aliyepo kwa sasa ni wa tatu.

"Wa kwanza (Edwin Mtei) aliongoza kwa miaka mitano tangu wakati huo 1993 hadi 1998 na kumwachia aliyefuata (Bob Nyange Makani) ambaye naye aliongoza kwa miaka mitano hadi mwanzoni mwa 2004 na kumwachia aliyepo sasa."

Ndipo waandishi waraka huo wanasema: "Huyu aliyepo (Freeman Mbowe) aliongoza kwa miaka mitano tangu mwaka 2004 hadi 2009 na kisha akachaguliwa tena mwaka 2009 kwa kipindi cha pili. Tunapenda kwa hatua ya mwanzo kabisa kutambua juhudi za wakuu wetu wote waliopita walizozifanya katika kuhakikisha taasisi yetu inakua kwa kutumia uwezo wote waliokuwa nao na katika mazingira yaliyowakabili.

### WAASISI CHADENA HAWAKUWA MADIKTETA

Waandishi wa waraka wanasema Mtei na Makani waliweka msingi mzuri ya kutong'ang'ania madaraka na badala yake kuachia mapema na kumwachia mwingine kidemokrasia bila vurugu.

"Hawakuwa madikteta na tunawapongeza sana. Walijitahidi sana kutokuwa wapenda madaraka na kimsingi walituwekea utamaduni ambao walitaka wote tuufuate na kujenga taasisi imara inayojali demokrasia na haki ya kila mwana taasisi."

Waandishi wa waraka wakazidi kuandika namna hii: "Lakini kuna matatizo yameanza kujitokeza na tusipochukua hatua haraka huko mbele tunaweza kupata shida kubwa. Tunapenda kuainisha matatizo hayo kwa uchache kama ifuatavyo:

Wakati tukiufanyia mwongozo wetu mabadiliko mwaka 2006 hatukugusa kipengele kinachomzuia kiongozi kuongoza kwenye nafasi moja kwa zaidi ya vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Lakini wakati mwongozo unachapwa chini ya uongozi uliopo, kipengele hicho kiliondolewa kinyemela. Mambo yanayotokea hivi leo yanaonyesha dhahiri kipengele hicho kiliondolewa kwa makusudi kwa maslahi na kwa faida ya viongozi waliopo madarakani kwa sasa.

Hiki kinaweza kuchukuliwa kama kitendo kidogo lakini kama viongozi wetu wanaweza kutokuwa waaminifu katika jambo kama hili, ni dhahiri hawawezi kuaminika na wanaweza kufanya mambo mengine makubwa na yenye athari zisizomithirika kwa taasisi yetu."

Ninachojadili hapa ni kwamba kukosekana kwa demokrasia ndani ya Chadema ndilo chimbuko la kuzaliwa kwa ACT-Wazalendo. Kwani ni kutokana na mkakati huo wa kutaka mabadiliko baadhi ya waliofukuzwa ikiwa ni pamoja na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Zitto Kabwe ambaye alikuwa kiongozi wa ACT-Wazalendo kabla ya kiujiuzulu hivi karibuni, aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, Profesa Kitila Mkumbo (sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji) na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Arusha, Samsoni Mwigamba.

Leo Chadema wanaweza vipi kufungua midomo yao mbele ya Zitto Kabwe, waliyemtimua kwa kuhisiwa kuwa anautaka uenyekiti wa chama hicho, kuwa wanadai demokrasia?

Kukosekana kwa demokrasia ndani ya ACT-Wazalendo, ndilo chimbuko la Kaka yetu mpendwa Prof. Kitilya Mkumbo (ambaye sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwezekaji) na wenzake kadhaa kujiuzulu uanachama wa ACT-Wazalendo na kujiunga na CCM; leo Zitto anawezaje kupata jeuri ya kudai demokrasia na kuruhusu yale yaliyojadiliwa kikaoni Zanzibar yaanikwe hata yawafikie Kitilya na wengineo waliokikimbia chama hicho?

### HALI IKOJE KATIKA VYAMA VINGINE?

Kukosekana kwa demokrasia ndani ya CUF ndilo lililokuwa chimbuko la kuzaliwa kwa Chama cha ADC; leo hii viongozi wa chama hiki ingawa nacho kimesambaratika watapata wapi ujasiri wa kuongea na waandishi wa habari juu ya maazimio yao ambayo yatamfikia Hamad Rashid wa ADC?

Kukosekana kwa haki na demokrasia ndani ya uliokuwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), ni kitu kilichomhangaisha sana Mzee Emmanuel Makaidi hata wengine kufikiria kwamba huenda ilichangia kifo chake cha ghafla; wale waliokuwa washirika wa UKAWA katika kikao cha Zanzibar, leo wanaweza vipi kufungua midomo ya kudai demokrasia mbele ya mtoto wa Mzee Makaidi (Oscar Makaidi), Mwenyekiti mpya wa NLD ambaye alirithi uongozi wa baba yake?

Kukosekana kwa demokrasia ndani ya NCCR-Mageuzi ndilo chimbuko la kuzaliwa Chama cha Chauma cha Mzee Hashim Rungwe; Leo Mbatia anaweza vipi kufungua mdomo wa kudai demokrasia mbele ya Mzee Hashimu Spunda Rungwe, aliyetimuliwa NCCR-Mageuzi kwa sababu tu alikuwa na mawazo tofauti na Mbatia?

Kukosekana kwa demokrasia ndani ya NCCR-Mageuzi ndilo chimbuko la viongozi wengi ndani ya Chama hicho kuukimbia uongozi wa Mbatia kwa kujiuzulu; wako wapi viongozi hawa; Mama yetu Edith Serafina Lucina, Polisya Mwaiseje, Ndimara Tegambwage, Dk Ringo Tenga, Japhet Hasunga, Mabere Marando, Anthony Komu, Joseph Selasini, Laurent Surumbu Tara, Mosena Nyambabe, Dk. George Kahangwa, Mama Zaituni Buyogera, Mama Leticia Mosore, Martin Juju Danda nk.

Mbatia ana uchungu gani na NCCR-Mageuzi hata adai demokrasia, na hali yeye ndiye alishirikiana na Chadema na CUF kukidhoofisha? Mwaka 2015 Mbatia alikuwa ndiye chanzo cha NCCR-Mageuzi kupoteza majimbo manne ya Kasulu Vijijini (Mama Zaituni Agripina Buyogera), Kasulu Mjini (Moses Joseph Machali), Kigoma Kusini (David Zacharia Kafulila) na jimbo la Muhambwe (Felix Francis Mkosamali).

Katika hali ya kushangaza alishirikiana na Chadema kuwatosa wagombea wote wa NCCR-Mageuzi walioteuliwa kugombea ubunge chini ya UKAWA na badala yake Chadema iliweka wagombea katika majimbo hayo na kumwomba marehemu Lowassa asiwanadi wagombea wa NCCR-Mageuzi waliopitishwa na UKAWA na badala yake awanadi wavamizi waliowekwa na Chadema. Hapa demokrasia ina nafasi kweli?

Mbatia aliyekwenda Zanzibar mwaka 2018 akiwa hana Makamu Mwenyekiti Bara, hana Katibu Mkuu wala Naibu Katibu Mkuu Bara, wote walimkimbia kwa sababu ya ugumu wa kushaurika. Leo anapata wapi ujasiri wa kudai demokrasia?

Je, mnakumbuka ya John Momose Cheyo na marehemu Amani Nzugile Jidulamabambasi kwenye UDP yao? Kwa sababu ilionekana ni dhahiri huwezi kumwondoa Cheyo kwa kura, ikabidi Jidulamabambasi na timu yake kufanya mapinduzi ambayo hata hivyo hayakudumu sana.

### KUDAI DEMOKRASIA NI SAHIHI LAKINI...

Ninaandika makala haya nikiwa sina mashaka moyoni ya kwamba, ni kweli kuna haja ya kudai demokrasia, suala la kufanya mikutano ya hadhara ni haki ya vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria kuu ya nchi (Katiba), pamoja na sheria ya vyama vya siasa.

Lakini hakuna uhalali na wala hakuna sheria yoyote inayosema; Chama chenye wabunge au madiwani ndicho tu kinaruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara, yeyote anayewaza katika mtazamo kama huu, anakwenda kinyume cha Katiba na sheria za nchi.

Hata vyama vyenye wabunge na madiwani havitakiwi kuifurahia hali hii kwa sababu; matamko kama haya pia yanavizuia vyama visivyo na wabunge na madiwani kwenye eneo fulani kufanya mikutano ya hadhara. Matamko haya yanawanyima wananchi haki ya kupata habari kama waliyopewa na Katiba ya nchi (Ibara ya 18 (b) na (d).

Kwamba ukiutaka uongozi kwenye vyama hivi vya upinzani ni kama unataka kuondoa sehemu ya kiungo cha kiongozi fulani anayeshikilia nafasi fulani! Vyama vimekuwa mali binafsi za watu. Leo eti watu hawa waliokaa madarakani kati ya miaka 20 hadi 32 nao wanalilia demokrasia kwa mkuu wa nchi, ambaye yupo madarakani kwa kipindi kifupi tu cha miaka mitatu sasa!

Yaani...!

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787au 0784 122 020.***



# ‘Nilikeketwa nikiwa na miaka 16, nimetesekaa sana’

**Na Mwandishi Wetu**

Alipokuwa akilelewa nchini Nigeria, Valerie Lomari anasema bibi alikuwa akimwonyesha upendo mkubwa.

Akiwa na umri wa miaka 16, alichukuliwa na bibi yake huyo hadi kijiji kingine akimwambia wanaenda likizo, ambako alijikuta akikatwa sehemu ya viungo vyake vya siri, jambo ambalo alijitahidi kulipinga bila mafanikio.

Licha ya uchungu aliopitia, sasa akiwa na umri wa miaka 52, tukio hilo la kukeketwa limekuwa kama nguo aliyoivaa mwilini muda wote iliyogoma kumwachia.

Valerie bado anaishi na kiwewe cha kihisia na kimwili kutokana na tukio hilo ambalo limekuwa na kasoro kubwa katika maisha yake na amedhamiria kutokomeza utamaduni huo kadri anavyoweza.

Mama huyo wa watoto watatu, sasa hivi husaidia waathiriwa wa ukeketaji huko Cambridgeshire, Essex, Hertfordshire na London. Haya hapa chini masimulizi yake.

“Nilipokuwa nikipita kwenye geti la nyumba hiyo, ghafla nilihisi kuumwa na tumbo. Mwanamke mmoja mrefu na mwenye sura ya kutisha alituingiza ndani na kufunga mlango.

Niliona visu, nyembe na bakuli lililokuwa na mafuta likiwa limewekwa juu ya meza, huku wanawake wengine wawili wakiwa wamekaa na kunikazia macho.

Nilimuuliza bibi kwa nini tulikuwa pale. Alifikiri kidogo kisha akaniambia anataka niwe msafi na kunitayarisha kwa ajili ya maisha ya ndoa.

Niligundua nini kitatokea na niliamua kupingana na bibi ambaye kwa kweli muda wote alikuwa na huruma kwangu isipokuwa siku hiyo. Nikataka waniache niondoke.

Hawakunikubalia. Nilipoona hawanielewi na sasa wanataka kunikeketa nilipiga kelele na kupiga mateke kwa nguvu zangu zote. Ghafla nilijikuta niko chini na wamenibana. Sikuweza kufurukuta.

Nilihisi maumivu makali na nikafikiri nitakufa. Nilipiga kelele hadi sauti ikawa haitoki. Nilimwona bibi yangu akiwa amesimama pembeni na akiniangalia kwa huruma, kisha akawa naye analia.

Nilihisi kusalitiwa na bibi yangu kipenzi. Alikuwa ni mtu pekee niliyempenda sana lakini alikuwa ameruhusu hili nifanyie jambo hili la kikatili.

Nililazimishwa kulala chini kwa saa kadhaa ili damu yangu isimame. Kwa kweli nilitokwa na damu nyingi sana. Baada ya siku mbili za kuwa katika nyumba hiyo, bibi yangu alinichukua hadi alipokuwa anaishi kule kijijini na nilikaa huko kwa muda. Nilijikuta kila mara ni mtu mwenye wasiwasi nyingi.

Mwishoni mwa majira ya joto, nilirudi shuleni nikasoma hadi nilipoingia chuo kikuu. Niliwaficha watu kilichotokea kwa sababu nilikuwa naona aibu, na nilidhani lilikuwa ni kosa langu kuwa mtu ambaye maeneo yake ya siri yamekatwa.

Wakati nikiwa mwaka wa mwisho chuoni, wakati huo nikiwa na umri wa miaka 26, nilikutana na mwanaume mbaye alikuja kuwa mume wangu Tony. Yeye alikuja akiwa ametoka London kumtembelea dada yake.

Sikumsemesha sana kwani nilikuwa na woga sana alipotaka niwe na urafiki naye lakini baada ya kuona amedhamiria kunioa, nilimweleza kila kitu kilichonipata. Nilitaka kumweka kando kwa sababu sikufikiri kwamba nilistahili kupendwa hadi kuolewa, lakini yeye aliedelea kunishawishi niwe mkewe.

Ingawa nilikuwa sipendi mtu mwingine pale chuoni wakiwemo wasichana wenzangu kujua kwamba nimekeketwa, lakini nilikuwa ninasikia habari za wasichana waliokeketwa jinsi wanavyochekwa na vijana wa kisasa. Kwamba wanapata taabu pale anapotoka na mtu wake kisha huyo jamaa akataka kupitisha vidole vyake sehemu zake za siri kwa sababu ataona tofauti.

Hata hivyo, ndani ya mwaka mmoja, Tony alihiari kufunga ndoa na mimi na kuhamia Uingereza. Hata tulipooana, ilikuwa vigumu kwangu kuongea naye, bado nilikuwa na wasiwasi mwingi. Nilikuwa nikizungumza naye kutoka chumba kingine au ningeandika maandishi asome kwenye kijikaratasi. Ilibidi aniamini lakini aliniamini zaidi ya nilivyojiamini.

Kushiriki tendo la ndoa daima ilikuwa vigumu kwangu hata baada ya kuolewa. Hata sasa nilivyolazimika kumridhisha mume wangu nilikuwa sisikii chochote kwa sababu na wakati mwingine inanifanya nijisikie kama mimi sio mwanamke kamili. Lakini najua nimebarikiwa kuwa na mtu ninayempenda.

Kwa bahati mbaya tulipoteza mimba nyingi kutokana na maambukizo niliyopata na yalinirudisha katika utoto wangu na maumivu yangu. Baada ya ile ya mimba ya tano kuharibika, mume wangu alinishawishi niende kwa daktari, lakini niliogopa sana kuruhusu mtu yeyote anichunguze. Nilidhani hata ningekamatwa. Lakini daktari wangu aliniunga mkono sana na kunielekeza kwa mtaalamu wa ukeketaji.

Ninashukuru sana kwamba tuliweza kupata watoto watatu wa ajabu pamoja, wasichana wawili na mvulana. Kuzaa kulikuwa na uchungu sana ingawa kwa wiki ya kwanza au zaidi sikuweza kushikamana na watoto kwa sababu nilikuwa nikiuguza majeraha.

Baada ya kupata mtoto wa tatu, nilipata ujasiri wa kuzungumza na bibi yangu kuhusu kile kilichotokea. Nilikata tiketi ya ndege na kurudi nyumbani. Nilimweleza yote niliyopitia na akaanza kulia. Ninaelewa sasa kwamba alifanya hivyo kwa upendo, alifikiri ilikuwa ni bora kwangu kwa sababu hata yeye alifanyiwa hivyo.

Alinitaka niwe mwazi kwa sababu na yeye ameshafunguka macho kwamba nizungumze juu ya uovu huo na kuhakikisha kuwa watu wanajua ukweli.

Nilianza kuwaambia watu juu ya kile kilichonipata na wanawake wengine waliniambia kwamba wao pia walikuwa wamepitia hayo. Miaka mitano iliyopita, niliamua kuanzisha shirika la Women of Grace, shirika linalounganisha waathiriwa wa ukeketaji na wale wenye matatizo ya kiafya tunawasaidia pia.

Tunakaribisha vikundi vya misaada, tunatengeneza nafasi salama na tunatuma wanawake kwa ushauri nasaha. Tunaelimisha familia na mimi huzungumza shuleni kuhusu hatari za ukeketaji.

Ukeketaji ni ukiukwaji wa haki za wanawake na unahitaji kukomeshwa kupitia elimu. Watoto wanapaswa kujua kwamba miili yao ni yao.

Nilikumbana na pingamizi mwanzoni kwa sababu eneo ninaloishi Essex wengi wao ni wazungu. Ukeketaji unaathiri zaidi jamii za wahamiaji nchini Uingereza, lakini pia unaweza kuathiri watu ambao wameishi hapa kwa miaka mingi.

Mara nyingi ukeketaji hufanywa nkwa kisiri. Wanafikiri ni jambo la kawaida na ni sehemu ya utamaduni au mila zao lakini hili ni janga. Kuna aibu nyingi na unyanyapaa na wasichana wengi hawataki kuzungumza yanayowapata kwa wale waliokeketwa.

Nimechapisha vipeperushi kuhusu FGM katika lugha tofauti ili niweze kuwafikia wanawake katika jamii zote.

Ninajivunia kuwa balozi wa Healthwatch Essex, kikundi ambacho kinalenga kuelimisha wengine kuhusu madhara ya ukeketaji ambayo humfanya mtu kuishi na kiwewe. Hivi majuzi nilitoa hotuba kuhusu FGM katika mkutano wa Umoja wa Mataifa huko New York.

Ninachotaka kusema ukeketaji ni kifungo cha maisha na bado ninaishi na kiwewe cha ukeketaji na kihisia. Lakini ninakataa kuiruhusu initeke nyara na kuamua mkondo wa maisha yangu. Nina nguvu na ninapendwa na sitaacha kusimulia hadithi yangu hadi utamaduni huu wa kikatili utokomezwe.


***Chanzo: BBC***







**MENEJA wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Kanda ya Kongwa, Amran Gama, akikagua aendeleo ya Mradi wa Chanzo cha Maji Sagara jijini Dodoma hivi karibu.**



**Chanzo cha Maji cha Sagara**

# Kongwa waanza kunufaika na maji ya chanzo cha Sagara

**Na Rahel Muhando, Dodoma**

KWA mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Kongwa iliyopo mkoani Dodoma, ina jumla ya wakazi 443,867.

Mahitaji ya majisafi katika Mji wa Kongwa ni mita za ujazo 2,400 kwa siku, ambapo uzalishaji uliopo ni wastani wa mita za ujazo 1,432 kwa siku.

Hadi kufikia Machi, mwaka huu, jumla ya wateja 1,892 walikuwa wameunganishwa na kufungiwa dira za maji kati ya wateja 76,200 wanaohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Kanda ya Kongwa.

Eneo la huduma kwa Mji wa Kongwa ni Kata nne ambazo ni Kongwa, Ugogoni, Sagara na Sejeli. Kanda ya Kongwa, ni eneo la huduma la Duwasa.

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa sasa ni asilimia 88 kutoka vyanzo vya maji vya visima na vyanzo vya maji mserereko.

Machi 15, mwaka huu, ni siku ambayo wananchi wa Mji wa Kongwa walianza kupata huduma ya majisafi na salama kutoka katika chanzo cha maji cha Mlima wa Sagara.

Chanzo hicho kipo wilayani Kongwa na kinachosimamiwa na na kuendeshwa na Mamlaka ya Majisafi na kinasimamiwa na Duwasa.

Chanzo cha maji mserereko kutoka mlima Sagara, kimekarabatiwa kwa gharama ya Sh. milioni 129 ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa kuzalisha lita milioni 1.32.

Mradi wa Sagara umekamilika na unahudumia idadi wa wananchi takriban 10,000 wa Vijiji vinne vya Ijaka, Ibwaga, Sagara A na B.

Mradi wa ukarabati wa chanzo cha maji ya mserereko cha Sagara, ulianza kutekelezwa na Duwasa Kanda ya Kongwa Agosti, 2023.

Maboresho ya chanzo cha maji ya Sagara, ni hatua mojawapo ya kuboresha hali ya huduma ya maji kwa Mji wa Kongwa pamoja na vijiji vya Ijaka, Sagara A na B, pamoja na Kijiji cha Ibwaga ambavyo vilikuwa na adha ya upatikanaji wa maji. Kazi zilizofanyika katika ukarabati wa mradi huu, ni pamoja na ujenzi wa choteo la maji katika chanzo, ulazaji na ufungaji wa bomba za maji za chuma zenye kipenyo cha inchi sita kwa umbali wa mita 432, ujenzi wa nguzo tisa za chuma katika korongo la Ibwaga na kuvusha bomba za chuma za inchi nne umbali wa mita 114 katika mto Ibwaga, ambapo ukarabati wake umefikia asilimia 98 na wananchi tayari wameanza kupata huduma ya majisafi ya mlima Sagara.

Mradi wa maji wa ukarabati wa chanzo Sagara, utasaidia jamii ya Kongwa kupata huduma ya maji yasiyo na chumvi, kuziba pengo la upungufu wa maji kwa kuongeza mita za ujazo 730 kwa siku, pamoja kukuza uchumi wa wananchi kwa kupata muda wa kutosha kufanya shughuli za kimaendeleo na kuimarisha afya za wananchi.

Katika kuimarisha dhana ya ushirikishwaji wa wananchi kwenye utekelezaji hadi kukamilika kwa miradi, Machi 21, mwaka huu ikiwa ni mwendelezo wa kuwapatia wananchi elimu ya utunzaji wa miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, Duwasa ilitekeleza jukumu hilo kwa wateja wake pamoja na kusikiliza kero kwa kauli mbiu isemayo: " Kero yako, wajibu wangu'.

Wananachi wa Sagara na Kongwa, kwa ujumla wanaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa Sh. milioni 129 kutekeleza mradi huu, ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kuwafikishia wananchi huduma ya majisafi na salama.

Meneja wa Duwasa Kanda ya Kongwa, Amran Gama, anasema Mradi wa Ukarabati wa Chanzo cha Maji cha Mlima Sagara, umepokelewa kwa shangwe na wananchi wa Kongwa kwani awali walikuwa wakipata maji ya visima ambayo yana asili ya kuwa na chumvi kiasi tofauti na maji wanayoyapata hivi sasa kutoka mlimani ambayo ni laini, baridi na matamu.

Aidha, Gama amewaomba wananchi wa Kongwa kujitokeza kwa wingi kuunganishiwa huduma ya majisafi baada ya mradi huo kukamilika, kwani maji ni ya ukakika.

Duwasa inasimamia na kuhudumia maeneo matano,ambayo ni Jiji la Dodoma na Miji ya Kongwa, Chamwino, Bahi na Kibaigwa.



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Kamati hizi zisilegelege kumaliza tatizo la ukatili



Nchi mbalimbali zinakabiliana na tatizo la vitendo vya kikatili, hususani ukatili wa kijinsia. Vita hii ni endelevu kutokana na ukweli kuwa vitendo vya kikatili vinazorotesha juhudi za kufikia maendeleo kuanzia ngazi ya familia, jamii na nchi kwa ujumla.

Kundi la wanawake na watoto ni muhimu katika juhudi za kujenga ustawi bora wa jamii na kujenga Taifa lenye maendeleo katika nyanja zote za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Pamoja na umuhimu wa kundi hili katika ustawi wa jamii na maendeleo, baadhi ya wanajamii wanashiriki kulifanyia ukatili kundi hili muhimu, hali inayoathiri juhudi zinazofanyika za kufikia ustawi na maendeleo ya nchi.

Ukatili unaotajwa ni pamoja na vitendo vya ukatili wa kimwili, ukatili wa kingono, ukatili wa kisaikolojia na ukatili wa kiuchumi.

Februari 15, 2022 jijini Dodoma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto Dkt. Dorothy Gwajima alitoa rai kwa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zinazotekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kuweka mikakati ya kupambana na vitendo vya ukatili vinavyotokea nchini.

Uundwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ni juhudi zinazofanywa na serikali katika mapambano dhidi ya vitendo vya kikatili kama vile ubakaji, ukeketaji, ulawiti, kuwapiga wanawake, ajira za watoto na mimba za utotoni.

Kutokana na umuhimu wa kujenga jamii yenye amani, furaha na ustawi, serikali haina budi kushirikiana na asasi za kiraia, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla katika vita dhidi ya vitendo vya kikatili.

Utendajikazi usioridhisha wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto hususani kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vijiji umetajwa kuwa miongoni mwa changamoto zinazoathiri mapambano ya ukatili wa kijinsia.

Kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zilizoko kwenye mitaa na vijiji ni nguzo muhimu katika utoaji wa taarifa za vitendo vya ukatili kwani ndizo kamati zinazoishi na wanajamii moja kwa moja. Kwa hiyo, ufanisi wa utendajikazi wa kamati hizi utasaidia hatua madhubuti kuchukuliwa dhidi ya wote wanaoshiriki katika vitendo vya ukatili wa wanawake na watoto.

Ongezeko la vitendo vya ukatili katika jamii umesababisha ongezeko la idadi ya kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Ongezeko la kamati za ulinzi ni jambo moja lakini ufanisi katika utendaji ni jambo la msingi zaidi kufanikisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Kwa hiyo, kamati zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi mitaa zinapaswa kuingia katika utendaji kazi uliotukuka ili malengo ya kupunguza kama si kumaliza kabisa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yaweze kutimia. Ni vyema kamati hizi zitekeleze kikamilifu wajibu wao ili kusaidia kujenga jamii yenye furaha, amani na ustawi bora kwa maendeleo endelevu.

Vitendo vya ukatili haviwezi kupungua kama kamati za ulinzi wa wanawake na watoto hazitasimama imara katika mapambano haya. Muda wa kamati hizi kukaa maofisi kusubiri taarifa za ukatili umepitwa na wakati, badala yake wanawajibika kufuatilia na kuchukua hatua dhidi ya ukatili au viashiria vyake.

Mafanikio ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yanachagiza kufikiwa kwa mipango ya maendeleo katika nchi yetu kutokana na umuhimu wa kundi hili katika jamii. Mathalani, mafanikio ya vita dhidi ya watoto wa mitaani, ukatili wa watoto, mimba na ndoa za utotoni zitawezesha watoto kupata haki yao ya elimu na hatimaye kufanikiwa katika masomo na maisha.

Wasichana ambao ni wanawake wa baadaye, wakipata haki ya elimu bila ubaguzi, watalea watoto wakiwapa misingi muhimu ya elimu, watajikomboa kifikra na kiuchumi na hatimaye Taifa kupata maendeleo.

Kamati za ulinzi wa wanawake na watoto nchi nzima zinapaswa kushirikiana na jamii ili kupata taarifa muhimu zitakazowezesha kupatikana kwa taarifa na hatimaye kuchukuliwa hatua dhidi ya wahusika wa vitendo vya ukatili.

Pia, jamii inawajibika kuwafichua wahusika wa vitendo vya ukatili ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi yao. Watanzania tuna wajibu wa kuifanya agenda ya mapambano ya vitendo vya ukatili kuwa ya kitaifa ili kila Mtanzania aone anawajibika katika kuchangia mafanikio na ustawi wa jamii kwa kuondoa vitendo vya kikatili.

Mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia pia hayapaswi kumsahau mtoto wa kiume ambaye naye yupo kwenye hatari ya kupoteza haki zake za kimsingi.

Mathalani, katika vituo vya mabasi, wapo watoto wengi wa kiume wanaofanya biashara ambao kwa umri wao walipaswa kuwa shuleni. Pia katika miji mikubwa kama Dar es Salaam watoto hao wanajishughulisha na shughuli za kuosha vioo kwenye magari pale magari hayo yanapokuwa katika foleni. Katika maeneo ya vijijini baadhi ya watoto waliopaswa kuwa shule unaweza kuwaona kwenye vibarua vya kulima mashamba, kuponda kokoto, kwenye shughuli za uvuvi na kadhalika.

Kwahiyo, kuna umuhimu wa jamii kubadilisha mtazamo wa kudhani kuwa mapambano ya ukatili wa kijinsia yanahusisha watoto wa kike na wanawake peke yao. Hata watoto wa kiume na wanaume nao wanafanyiwa vitendo vya kikatili, hivyo ni muhimu katika utekelezaji wa mikakati, wasisahaulike ili kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia na hatimaye kujenga jamii imara yenye furaha na amani.

*Mwandishi ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoni Dodoma.*



KLINIKI YA FIKRA



# Mpango wa maendeleo yako binafsi

MPANGO wa Maendeleo Binafsi (Personal Development Plan) ni mwongozo kwa maisha na mafanikio yako ya baadaye. Maendeleo binafsi ni mchakato wa mtu kujiboresha mwenyewe kupitia tabia na shughuli zenye malengo.

Ni harakati ya kukua kibinafsi ili kuongeza ubora wa maisha yako na kufikia ndoto na matarajio yako. Unapoamua kuunda mpango wa maendeleo binafsi, maana yake unaanza kutafakari juu ya aina ya mtu unayetaka kuwa, ujuzi unaoutamani, na mafanikio unayotaka.

Mtu hawezi kuwa zaidi ya uwezo wa fikra zake. Kwa maana nyingine, mtu unayemwona ni zao la fikra zake. Unapoamua kuchukua udhibiti juu ya fikra zako, unaweza kuongoza maendeleo yako binafsi na kuharakisha kufikia unachotaka. Kuweka malengo ya maendeleo binafsi, kunafungua ulimwengu wa fursa mpya kwako na kuongeza ubora wa maisha yako.

Kuna tofauti kidogo kati ya maendeleo binafsi (Personal Development) na maboresho binafsi (Self Improvement). Maendeleo binafsi ni kazi unayofanya kubadilisha mwonekano wako. Ni juhudi unazofanya kuendelea katika kazi yako, mtindo wako wa maisha, mtazamo wako, umbo lako, na uhusiano wako na watu.

Kwa upande wa pili, kujiboresha kibinafsi ni mabadiliko ya ndani kuelekea ubora wa tabia, hadhi, au maarifa kwa jitihada zako wenyewe. Huu ni mchakato wa maisha wa kudumu wa kutafuta njia za kubadilisha tabia zako ili ufikie uwezo wako mkamilifu.

## MAENEO SABA YANAYOONESHA MAENDELEO BINAFSI

Maendeleo binafsi lazima kuzingatia mambo ya msingi kama vile ujuzi binafsi, ukuaji binafsi, nguvu binafsi, nk. Mambo haya pamoja na mengine, huunda tabia za kujiboresha mwenyewe wakati ukuaji wa kibinafsi unategemea sana elimu na ujuzi. Kuna maeneo saba makuu ya maendeleo binafsi: - **Ujuzi binafsi** – Huu unaweza kuwa ule uliozaliwa nao pamoja na ule uliopatikana kupitia kujifunza na mazoezi ya makusudi. Mifano ya ujuzi wa binafsi unaotakiwa kuwa nao ni kama vile ujuzi wa kufanya maamuzi sahihi, ujuzi wa kufanya kazi kwa ushirikiano, ujuzi wa kuwa na utaratibu, ujuzi wa mawasiliano, na ujuzi mwingine muhimu.

**Ukuaji binafsi** – Hii inaanza na kuwa na mpango wa ukuaji binafsi. Ni hatua za kuelekea kuwa bora zaidi na kutoka katika eneo lako la faraja (Comfort Zone).

Binadamu na akili ya binadamu vinabadilika kila wakati. Huwezi kuwa mtu yuleyule uliyekuwa mwaka mmoja uliopita. Hii ni jitihada ya kuwa toleo bora zaidi la wewe leo kuliko ulivyokuwa jana.

**Nguvu binafsi** - Ni mamlaka ambayo wengine wanakuamini kuwa nayo katika hali fulani. Nguvu hii inachochewa na uwezo wako wa mawasiliano, maarifa yako, na hali yako kimwonekano.

Nguvu hii inaweza kuzidishwa na mtandao mpana zaidi wa mawasiliano, kutafuta kujifunza zaidi, na kukua kifedha. Nguvu hii inazidisha idadi ya milango ambayo wengine wataiacha wazi ili wewe uingie.

**Maboresho binafsi (Self Improvement)**- Kujiboresha binafsi ni kujenga tabia njema na kuwa na mtazamo chanya wa kiakili. Kufikiria kabla ya kuchukua hatua, ni muhimu sana katika kukuza kiwango kikubwa cha kujiboresha binafsi. Ili kukusaidia kufikiri, weka vipaumbele na kuwa na mtazamo chanya wa kiakili ili kufikia malengo yako.

**Uwezo binafsi** - Uwezo binafsi unawezakuwa sawa na nguvu Binafsi, isipokuwa uwezo ni nguvu unayoiona ndani yako, badala ya jinsi wengine wanavyokuona. Kukuza taswira chanya na kukumbatia ubunifu katika maisha yako ya kila siku kunaweza kuharakisha muda wa kufikia uwezo binafsi na malengo yako.

**Tathmini binafsi** - Ni muhimu kufahamu maeneo ambayo una vipaji asili pamoja na kuchambua maeneo ambayo unahitaji kujiboresha. Hii inaitwa tathmini binafsi.

Hapa unatakiwa kuwa mwaminifu kuhusu hali yako ya sasa, kwa kuwa hiyo pekee ndiyo hatua ya kwanza kuelekea mbele. Mara kwa mara jitajidi kujitathmini na kuona maeneo yako ya mapungufu na kufanya marekebisho kwenye mapungufu yako huku ukiimarisha maeneo yako ambayo una nguvu na ubora.

**Malengo binafsi** - Ndoto hazina maana bila malengo yaliyo wazi. Kuweka malengo ya muda mfupi na mrefu ni hatua muhimu katika kuyatimiza na kukua. Kuwa na mpango uliowekwa kunakusaidia kuelewa vyema ni mikakati gani inayohitajika.

Kama unapenda kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi Binafsi au ya Serikali, Kikundi cha kijamii, Kanisa, Umoja, NGO, Mtu binafsi n.k) Karibu tuwasiliane

*Wework Consult - Your Partner in Growth.*



Na Hamisi Kibari
Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 24



**Licha ya kusamehewa na watu ambao wangekuwa mashahidi kwa kusema hawana mpango wa kumshitaki, Chris anapofikishwa mahakamani anakiri kosa la kumuua mkewe bila kukusudia. Lakini siku ya hukumu ghafla mkewe huyo ambaye alijua alikufa anatokea na watu wengi wanashangaa na kusababisha tafrani mahakamani wakidhani ni msukule. Dk. Goima anaieleza mahakama kilichojiri. Anaeleza sababu ya kumdanganya Chris kuhusu kifo cha mkewe ni kuudhiwa na tabia yake na hasa aliposikia masimulizi ya mkewe na kuanza kumchuna fedha ili kumkomoa…. Endelea.**

"Mh… Kitendo cha kuniletea mwanamke chumbani kwangu, kunipiga mithili ya kuniua na kutaka nisijulikane kama nimekufa na kuzikwa kama mzoga na halmashauri ni kwamba mimi hanipendi kabisa na siwezi kulazimisha mapenzi," alisema na watu wengi mahakamani pale wakamgeukia Chris ambaye machozi yalikuwa yanamwagika. Chris akiwa bado kasimama kizimbani mithili ya mtu aliyemwagiwa maji alinyoosha mkono kutaka kusema kitu.

Jaji alimruhusu lakini alipotaka kuzungumza akajikuta analia.

Jaji aliandika maneno mawili matatu kisha akanyanyua tena uso wake. "Kwa maelezo hayo na kwa mujibu wa kesi ya kuua bila kukusudia iliyokuwa mbele yangu, ninamwachia huru mshitakiwa Chrysostom Mataruma Magati. Lakini anaweza kushitakiwa kwa kosa la kujeruhi… Hata hivyo, wewe dokta na Tausi, mnaweza kushitakiwa pia kwa kudanganya kifo cha mtu na kusababisha kesi hii ambapo gharama nyingi za serikali zimetumika... Hilo ni suala la polisi wakiona inafaa. Hata mauziano yenu ya nyumba kwa mbali ninaona kama kuna utata wa kisheria. Lakini binafsi nadhani mlifanya vyema kumtia adabu mwanamume wa hovyo kama Chris…"

Baada ya kusema maneno hayo, Jaji Wesai alinyanyuka, na watu wote walinyanyuka pale mahakamani. Mwalimu Misango akitokwa machozi ya furaha alikuwa wa kwanza kumrukia Tausi na kumkumbatia huku Jacob naye akisubiri zamu ya kumkumbatia dada yake.

Chris akiwa huru baada ya kuamini siku hiyo angelifungwa, na akiwa kama asiyeamini yale yaliyotokea mbele yake, alikwenda na kumpigia magoti Tausi.

Dada yake na Jacob waliokuwa pale wakaamua kumpisha na kusimama pembeni.

"Mke wangu. Kwa kweli nilikukosea sana. Nisamehe. Nisamehe kwa yote. Naomba tuungane tena kwa sababu ya watoto wetu hata kama hunipendi tena," alisema Chris.

"Kwanza usiniite mke wako. Mke gani unampiga mithili ya kifo halafu unatelekeza maiti yake hospitali. Wewe ni mnyama. Hilo la mimi kuishi na wewe kama mtu na mke, sahau. Haliwezekani. Lakini pamoja na yote, leo ninapenda tu nikuambie kwamba nimekusamehe. Nyanyuka na wala usinipigie magoti. Haya yamekwisha lakini ujue kinachofuata ni kuachana tu kwa wema. Mimi siwezi tena kuishi na wewe kama mume na mke hata sekunde moja zaidi ya kushirikiana tu kulea watoto wetu," alisema Mama Kenny."Ninakupenda mke wangu. Nisamehe sana…""Mke wako? Hapana. Mimi si mke wako tena bali mzazi mwenzako. Na hayo mapenzi yamekuja lini? Ni baada ya yule kimada wako kukukimbia? Ni baada ya kukufilisi? Kwa mfano nikiamua tuishi tena pamoja, hivi ukipata kimada mwingine itakuwaje na mabinti warembo wanazaliwa kila kukicha… Hapana. Nimeshaamua, nitaolewa na Dk. Goima na kila kitu kinakwenda vyema kwa ajili ya ndoa."

"Rudisha moyo wako mke wangu. Unajua…"

"Nimeshakwambia usiniite tena mke wako. Niite Mama Kenny. Kwanza mimi nimebadili dini. Nitaolewa na Muislamu mwenzangu, unasikia?"

"Hilo la dini tutalizungumza. Tutafikia tu makubaliano," alisema Chris akiwa bado amepiga magoti.

**Nisamehe Mama Kenny. Shetani tu. Tuanze upya tulee watoto wetu... Unaweza ukawa kweli hunipendi tena lakini kwa niaba ya watoto wetu naomba turudi kuishi kama zamani.**

"Nyanyuka usipoteze muda wako."

"Nisamehe Mama Kenny. Shetani tu. Tuanze upya tulee watoto wetu… Unaweza ukawa kweli hunipendi tena lakini kwa niaba ya watoto wetu naomba turudi kuishi kama zamani," alizidi kuomba Chris akiwa bado kapiga magoti na sasa machozi yakiwa yanamtoka."Watoto watalelewa tu, lakini tukiwa hatuko pamoja… Ninajua wanaume mnafanana kwa aina fulani lakini nadhani Dk. Goima atanifaa na ananipenda. Unachotakiwa kufanya ni kunipa talaka yangu nikuache utange na njia na akina Joyce wako," alizidi kusema Mama Kenny."Usiseme hivyo Mama Kenny… Usiseme hivyo…"

"Itabidi ukubaliane na matokeo Chris. Penzi langu kwako halipo tena. Nilikupenda sana lakini wewe ndiye mtu ninayekuchukia pengine kuliko mtu yeyote hapa dunia. Ona umefanya niishi mbali na wanangu kwa muda wote huu. Mwanaume laana kabisa," alisisitiza Tausi na mara Dk. Goima akaja pale akiwa ameandamana na mkewe na yule mwanamke akamshika mkono Tausi ili waondoke. "Huyu ndiye shemeji mpya," aliuliza Jacob ambaye muda wote alikuwa kimya akisikiliza malumbano ya dada yake na mumewe."Ndiye huyu kaka ytangu," alisema akianza kupiga hatua."Mama Kenny, ninajua mdogo wangu alikutendea mabaya. Lakini mbona umefanya haraka sana. Ungempa nafasi nyingine," alisema Mwalimu Misango akimfuata nyuma."Unasema kweli wifi… Lakini mambo haya hupangwa na Mungu. Naona ndiye kanipangia haya. Angepanga nife kwa kipigo cha mdogo wako ningeshakufa. Ningeweza hata kufa kwa machungu ya kutelekezwa na mdogo wako. Ningeweza hata kufa kwa presha siku nilipokuta kondomu kwenye suruali yake. Hukumbuki wifi… Nitakuja nyumbani kuwachukua wanangu. Ninakushuru sana na wewe nsitokutenga abadani wifi. Ninakupenda sana," alisema akiondoka na kujongea kwenye gari la kifahari la Dk Goima. Alimuaga kaka yake, Jacob akamweleza kwamba atawasiliana naye baadaye.

"Sawa dada tutawasiliana. Na mimi kimsingi ninaheshimu matakwana uamuzi wako."

Chris alinyanyuka akimwangalia mkewe akijongea kwenye lile gari jeusi lililokuwa limeegeshwa pembeni ya mahakama hiyo. Kama asiyeamini macho yake akaona mkewe akimezwa na hilo gari.

Gari lile jeusi, jipya likaondoka. Chris akabaki akifuta machozi pale nje ya mahakama.

"Haiwezekani… Haiwezekani," akajisemea kama mtu aliyepagawa.

"Twende nyumbani Chris… Tuliza Mawazo. Haya ndio mavuno ya kutelekeza familia."Mwisho

# DRC yamteua Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke

**DRC, Congo**

WAZIRI wa Mipango wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Judith Suminwa Tuluka, amekuwa Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke katika taifa hilo la Afrika ya Kati, televisheni ya serikali imetangaza.

Waziri huyo Mkuu mpya, ni mchumi na amechukua nafasi ya Jean Michel Lukonde, kufuatia ushindi wa kishindo wa muhula wa pili wa Rais Felix Tshisekedi, kwenye uchaguzi wa Desemba 20, mwaka jana.

Tuluka alisema kupitia televisheni ya taifa: “Kazi ni kubwa, changamoto ni kubwa, lakini kwa pamoja tutafika.”

“ Ninafahamu jukumu kubwa linalonisubiri,” aliongeza, akisema anataka kufanya kazi “kwa ajili ya amani na maendeleo” ili “wananchi wa Congo wanufaike na rasilimali” za nchi.

Rais Felix Tshisekedi, alishinda rasmi kwa asilimia 73.47 kwenye uchaguzi wa Desemba, mwaka jana ambao ulifanyika kwa amani kwa kiasi kikubwa katika nchi inayokumbwa na ghasia na ukosefu wa usalama.

Lakini upinzani ulidai uchaguzi uligubikwa na udanganyifu.

Waziri Mkuu mpya atakuwa na jukumu la kutekeleza vipaumbele vilivyotangazwa na Rais kuhusu ajira, vijana, wanawake na uwiano wa kitaifa katika taifa hilo la takriban watu milioni 100.

Rais Tshisekedi alishika madaraka tangu mwaka 2019 akiahidi kuboresha maisha nchini DRC, nchi yenye utajiri wa madini, lakini yenye raia wengi maskini na kumaliza umwagaji damu wa miaka 25 mashariki mwa nchi.

VOA.



Judith Suminwa Tuluka, Waziri Mkuu mpya wa DRC

# Watoto 9 wafa kwa kulipukiwa bomu la kutegwa ardhini

**AFGHANISTAN, Taliban**

TAKRIBAN watoto tisa wamefariki dunia baada ya bomu la kutengwa Ardhini kulipukaa usiku, Maafisa wa Taliban Kusini Mashariki mwa Afghanistan wamesema.

“Bomu lililokuwa halijalipuka” lilikuwa ni mabaki ya mizozo ya zamani, lililipuka siku ya Jumapili wakati kikundi cha watoto wa kiume na wa kike wakilichezea katika Wilaya ya Geru, Jimbo la Ghazni, alisema Msemaji wa serikali ya jimbo.

Hamidullah Nisar, alidai kuwa bomu hilo liliachwa wakati wa uvamizi wa Russia nchini Afghanistan katika miaka ya 1980.

Umoja wa Mataifa mjini Kabul ulisema Jumatatu kuwa maelfu ya raia, wakiwemo wanawake na watoto, nchini Afghanistan waliuawa au kujeruhiwa na mabomu ya kutegwa ardhini na vilipuzi vingine vilivyobakia baada ya vita.



Ilibandika katika mtandao wa X, ambao awali ulijulikana kama Twitter, kuwa UN “Washirika wa MinAction walikuwa wameondoa mabomu eneo la kilomita 3,011,” wakisisitiza kuwa kazi zaidi inahitajika kuwalinda Waafghanistan, ikitokana na miongo kadhaa ya migogoro.

Afghanistan imepitia miaka kadhaa ya vita vya wenyewe kwa wenyewe miaka ya 1990 baada ya majeshi ya Russia kuondoka nchini, na kumaliza kipindi cha muongo mmoja wa uingiliaji kati wa kijeshi nchini humo.

Wataliban wenye misimamo mikali, waliibuka washindi katika mapambano ya kuchukua madaraka kati ya vikundi mbalimbali vya Afghanistan, wakichukua udhibiti wa sehemu kubwa ya nchi hiyo mwaka 1996 na kuitawala kwa kutumia tafsiri yenye msimamo mkali ya Sheria za Kiislamu.

Watawala wenye msimamo mkali waliondolewa madarakani miaka mitano baadae wakati Marekani na washirika wake walipoivamia Afghanistan kuwaadhibu wale waliokuwa wanawahifadhi al-Qaida waliopanga shambulizi la kigaidi la Septemba, mwaka 2001 katika miji ya Marekani.

VOA.


**YERUSALEM, Israel**

# Israel kuzuia matangazo ya Al Jazeera

BUNGE la Israel limeidhinisha sheria inayoipa serikali mamlaka ya kupiga marufuku matangazo ya chaneli za TV ikiwemo Al Jazeera, mtandao unaomilikiwa na taifa la Qatar.

Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, alisema: “Atachukua hatua mara moja,” ili kufunga ofisi ya ndani ya mtandao huo.

Marekani ilionyesha wasiwasi wake kuhusu hatua hiyo. Huku waandishi wa habari wa kigeni wakipigwa marufuku kuingia Gaza, wafanyakazi wa Al Jazeera walioko kwenye ukanda huo wamekuwa baadhi ya waandishi pekee walioandika habari za vita hivyo mashinani.



Bunge la Knesset, Bunge la Israel, liliidhinisha muswada huo unaoruhusu mitandao ya kigeni inayozingatiwa kuwa tishio kwa usalama wa taifa kupigwa marufuku kwa muda. Marufuku hiyo ingewekwa kwa muda wa siku 45 kwa wakati mmoja, ambayo inaweza kuongezwa upya.

Sheria hiyo itaendelea kutumika hadi Julai au hadi mwisho wa mapigano makubwa huko Gaza. Al Jazeera haitatangaza tena kutoka Israel, Waziri Mkuu Netanyahu aliandika kwenye Twitter/X, akiuita mtandao huo “chaneli ya kigaidi”. Kwa miaka mingi, maafisa wa Israel wamekuwa wakishutumu mtandao huo kwa chuki dhidi ya Israel. Lakini ukosoaji wao kwa shirika hilo la utangazaji umeongezeka tangu mashambulizi ya Hamas ya Oktoba 7, mwaka jana.

Mamlaka zinadai kuwa ina uhusiano wa karibu na Hamas, lakini Al Jazeera inakanusha vikali.

Katika taarifa, Al Jazeera ilisema: “Netanyahu hakutoa sababu za haki kwa ulimwengu kwa mashambulizi yake yanayoendelea dhidi ya Al Jazeera na uhuru wa vyombo vya habari isipokuwa kuwasilisha uongo mpya na kashfa za uchochezi dhidi ya mtandao na haki za wafanyakazi wake. BBC.

**VITA VYA ISRAEL, GAZA:**

# Israel yadaiwa kuwaua Majenerali wa Iran

**TEHRAN, Iran**

KIKOSI cha Walinzi wa Mapinduzi nchini Iran (IRGC), kimesema maafisa saba wameuawa katika shambulizi la Israel katika jengo la Ubalozi Mdogo wa Iran katika mji mkuu wa Syria, Damascus.

Brigedia Jenerali Mohammad Reza Zahedi, Kamanda Mkuu wa Kikosi cha wa Wasomi cha Quds na Brig-Jenerali Mohammad Hadi Haji-Rahimi, Naibu wake, walitajwa miongoni mwa waliofariki dunia.Serikali za Iran na Syria, zimelaani shambulizi hilo ambalo liliharibu jengo jirani na Ubalozi wa Iran.

Jeshi la Israel lilisema halizungumzia taarifa za vyombo vya habari vya kigeni. Hata hivyo, limekiri kutekeleza mamia ya mashambulizi katika miaka ya hivi karibuni kwa kuyalenga makundi ambayo yana uhusiano na Iran nchini Syria na makundi washirika yenye silaha ambayo, yanayofadhiliwa na kupewa mafunzo na Walinzi wa Mapinduzi.

Mashambulizi ya Israel yameripotiwa kuongezeka tangu kuanza kwa vita huko Gaza Oktoba, mwaka jana, kujibu mashambulizi ya kuvuka mpaka Kaskazini mwa Israel yaliyofanywa na Hezbollah na makundi mengine yanayoungwa mkono na Iran huko Lebanon na Syria.

Lakini shambulio la Jumatatu litaonekana kama ongezeko kubwa la mashambulizi hayo.

Waisrael wanaonekana kujaribu azma ya Wairan na washirika wao na kuashiria kwamba wana nia ya dhati ya kuongeza shinikizo kwa maadui zao.

Waisrael wanaangalia ukweli kwamba Iran na Hezbollah, hazijafanya bidii kama ambavyo wengine wanaweza kutarajia. Sasa wanataka kuona iwapo Iran na Hezbollah watachukua hatua yoyote dhidi ya Israel.

BBC.



**Mashambulizi ya Israel yameripotiwa kuongezeka tangu kuanza kwa vita huko Gaza Oktoba, mwaka jana.**

# Timu za vijana zisiwe kiini macho

## >>> Tukiziendekeza Simba, Yanga tutavuna mabua
## >>> Iliwezekana kwa kina Manara, kwa nini isiwe sasa?





**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kutoa mshangao wake juu ya kitendo cha Shirikisho la Soka nchini (TFF) kubariki kuongeza idadi ya wachezaji wa kigeni kwenye timu za Ligi Kuu ya NBC kutoka 10 hadi 12.

Akizungumza baada ya mbio za marathoni za maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Juni 25 mwaka jana, Dk. Kikwete alisema kuwa, wakati idadi ya wachezaji wa kigeni wanaoruhusiwa kucheza soka ikiwa ni 8 aliwahi kushauri ipunguzwe alipoalikwa kwenye sherehe za klabu ya Yanga huko nyuma.

"Lakini badala ya kupunguza wachezaji hao wa kigeni, majibu waliyotoa ni kuongeza kutoka idadi hiyo ya wachezaji nane hadi 12!

Mnasukumwa na klabu za Simba na Yanga, hizi klabu zinajali ushindi tu na si kuwekeza kwa watoto na vijana," alinena Dk. Kikwete huku akimtaka Naibu Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Hamis Mwinjuma aliyekuwepo kwenye shughuli ile kwenda kukaa na TFF kuliangalia hilo.

Mimi kwa upande wangu sina tatizo na idadi hiyo ya wachezaji wa kigeni kwenye ligi yetu, lakini naungana na Dk. Kikwete kwa jambo la kutoziendekeza klabu za Simba na Yanga zinazokumbatia wachezaji hao wa kigeni, bali naisihi TFF, vilabu vingine na wadau mbalimbali wa soka wajikite kwenye kuandaa watoto na vijana wa kuja 'kuwakimbiza' wachezaji hawa wa kigeni.

Kama jambo hili liliwezeka huko kwenye miaka ya sabini hadi tisini, kwa nini lishindikane hivi sasa ambapo kuna fedha za kutosha kupitia wadhamini na wafadhili, miundombinu mizuri kuanzia pale TFF hadi kwenye taasisi binafsi?

Na isiishie kuwaandaa na kisha kuwatelekeza wakifika umri fulani, bali kuwe na mwendelezo wa kuwatunza wachezaji wote wanaoandaliwa kwenye timu zetu zote za vijana na si kama ilivyo sasa ambapo wanasoka wengi chipukizi hupotelea kusiko julikana!

Dk. Kikwete alisema klabu hizi kubwa zinajali ushindi tu, mimi naongeza kwamba zinaangalia na kuvuna fedha kwa njia za mkato pia. Ndiyo, kwa sasa watu wanachojali ni pesa tena za dili kuliko ilivyokuwa huko miaka ya nyuma.

Leo hii huwezi kuona timu zetu zikiwa na vituo vya soka au michezo kwa ajili ya vijana wetu kama ilivyokuwa zamani. Zipo timu za kiinimacho zinazoitwa vikosi B!

Kiinimacho? Ndiyo, kwa sababu sheria za kushiriki Ligi Kuu zinalazimisha klabu kuwa na timu za vijana, basi viongozi huokoteza wachezaji mitaani tena wakati mwingine bila kujali umri sahihi unaotakiwa ilimradi wakidhi matakwa ya TFF na ligi ikimalizika ndiyo huwa mwisho wa hizo timu za vijana!

Matokeo yake ni nini? Ni kunufaika kwa klabu zenye nguvu ya fedha hapa nchini, lakini kuzorota kwa soka letu ngazi ya taifa kiujumla, ingawa sina budi kupongeza uongozi wa sasa wa TFF chini ya Wallace Karia unavyopambana kuinua kandanda letu.

Watanzania bado wanakumbuka wakati wa Utawala wa Awamu ya Pili pale kiongozi wetu, hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi alipo sema kuwa Tanzania kisoka ni kichwa cha mwenda wazimu.

Alilisema hilo baada ya kuona Tanzania ikifungwa na hata na timu kutoka kwenye mataifa ambayo idadi ya watu wao



>>>Inaendelea Uk. 21

# Timu za vijana zisiwe kiini macho

>>>Inatoka Uk. 20

haizidi laki tatu kama vile Swaziland kwa miaka ile.

Uongozi wa Karia na Katibu wake Mkuu Wilfred Kidau hawa wanastahili pongezi kwa kutilia mkazo soka la vijana na lile la wanawake, lakini kote duniani hivi vyama vya soka ni watoa sera tu, wanaotakiwa kwa kiwango kikubwa kuinua soka letu ni huku ngazi ya vilabu ambako ndiyo kwenye timu na wachezaji.

Leo hii nchi kama Burkina Faso iliyoko Magharibi mwa Afrika ikiwa haina ardhi ya kutosha kuanzia ya kulima mpaka ya kucheza soka, lakini hivi sasa imejiyakinisha kuwa si kichwa cha mwenda wazimu. Burkina Faso ambayo huko miaka ya nyuma ilikuwa nyuma kisoka, kwa sasa ni hatari kulio baadhi ya nchi nyingi ikiwemo Tanzania.

Mafanikio kama hayo yanatokana na mipango mahsusi ya kizalendo zaidi kuliko ile ya kidili kama inavyojizatiti hapa kwetu kwa sasa.

Hivi, ni nini kilichofanya au kinachofanya timu kama Young Africans maarufu Yanga na Simba kutokuwa na programu endelevu za vijana wadogo kama ilivyokuwa kwenye miaka ya sabini?

Wachezaji kama Adolph Rishad, Juma Pondamali, Mohamed Mkweche, Mohamed Yahya 'Tostao' , Sunday Manara, Kassimu Manara, Leodgar Tenga na wenzao kama hao ni zao la timu za vijana la Yanga wakati huo. Huku kwa watani zao Simba kulikuwa na akina Willy Mwaijibe, Nicco Njohole, George Kulagwa, Abasi Kuka, marehemu Ramadhan Lenny na wengine kadhaa walioandaliwa kwenye timu za vijana.

Siyo Dar tu hata huko mikoani kulikuwa na utaratibu wa kuandaa vijana ambao baadaye walikuja kuwa tegemeo siyo kwa klabu kubwa bali hata taifa pia.

Baadhi ya wachezaji hao ni kina Sembwana, Mbwana Abushiri, Hed Seif na mdogo wake Rashid Seif, Washokera wote kutoka Tabora.

Baada ya hao walikuja kina Zamoyoni Mogela aliyepewa jina la "Golden Boy" na aliyekuwa mtangazaji mashuhuri wa soka hapa nchini marehemu Ahmed Jongo.

Alikuwepo Gibson Sembuli, Ramadhani Mnyepe, Khalid Bitebo, Mwinda Ramadhani. Huyu alifanya makubwa katika soka ya Tanzania mpaka akaitwa "Mwinda Maajabu" kwa jinsi alivyokuwa akisakata soka kwa umahiri wa kutopea.



Hawa ni kuwataja wachache tu kwani wako wengi akiwemo Khalid Abeid maarufu kama "Mpishi" kwa jinsi pasi zake murua zilivyokuwa zikiwaunganisha wachezaji wenzake wa nafasi za mashambulizi waliopata mabao kama kumsukuma mlevi.

Kwa mtaji huu kwa nini TFF isitayarishe sheria au muswada maalum wa kuwataka wanaoanzisha timu tangu za soka kuwa na vituo vya wachezaji wadogo ambao watalelewa hapo hadi wanafunzi na kuwa kama kina Pondamali?

Nathubutu kusema hivi kwa sababu katika kipindi hiki ambapo soka imepewa uwezo mkubwa wa kuwa na wafadhili wa nguvu kama kina Mo, Azam GSM na wengine, lazima soka itakuwa kwa kiwango kikubwa.

Soka yetu itakapokuwa kwa kiwango hicho vijana wetu nao watapata nafasi ya kucheza nje na kuongeza pato lao na la Taifa badala ya sisi kuwa walezi wa wanasoka kutoka nje ambao rekodi zao hazijulikani wala kutambulika.

Kuna tetesi kubwa kwamba hao wanaojifanya madalali wa kuwaleta wachezaji hao hapa nchini ni wapiga dili tu na wala si chochote katika tasnia hiyo, ndiyo maana rundo la wachezaji hao ufeli kuliko wale wanaofanikiwa hapa Tanzania.

Kwa muktadha huo, naungana tena na Dk. Kikwete tutupie zaidi jicho kuwaendeleza watoto na vijana wetu ambao ndiyo itakuwa 'mwalobaini' wa kutoendekeza hawa wachezaji wa kigeni, yaani tukiwa na wachezaji wenye viwango bora na kukidhi sifa zote za kisoka, hawa wageni watakimbia wenyewe!

Binafsi nakumbuka jinsi timu ya Simba iliyofika nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika mwaka 1974 huku ikiwa na wachezaji wote Watanzania, pia ile iliyofika fainali ya Kombe la CAF mwaka 1993 ikiwa na wachezaji wazalendo watupu sambamba na ile iliyotinga Ligi ya Mabingwa (Nane Bora) mwaka 2003 ambayo ilikuwa na mchezaji mmoja tu wa kigeni, marehemu Ramadhani Wasso.

Yanga ya akina Kitwana Manara, Abdulhaman Juma, Hassan Gobos, kipa mahiri Patrick Nyaga na wengine kadhaa ilifika hatua ya robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika mwaka 1969 na 1970 ikatolewa kimizengwe kwa kurusha shilingi baada ya sare kwenye mechi zote mbili za nyumbani na ugenini dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana!

Hata ile Yanga iliyotinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 1998 ilisheheni wachezaji wazalendo watupu walioandaliwa barabara tangu wakiwa kwenye umri mdogo.

Aidha, bado nakumbuka jinsi timu ya Pamba FC maarufu kama Wana-TP Lindanda iliyokuwa na wachezaji wazalendo watupu walipoifunga timu ya Anse- aux- Pins FC ya Seychelles jumla bao 17- 1 kwenye michuano ya Kombe la Washindi mwaka 1990, baada ya kushinda ugenini bao 5-0 na kuja kumalizia kazi kwenye mechi ya marudiano pale CCM Kirumba kwa kuishindilia timu ile bao 12-1.

Ushindi ule wa Pamba ndiyo rekodi kwa timu zote za Tanzania na Afrika kwa ujumla kwa ushindi mkubwa hadi hivi sasa!

Narudia tena tusiziendekeze hizi klabu kongwe za Simba na Yanga, zina nguvu sana kwenye medani ya soka la nchi hii, tusipoangalia hili tutavuna mabua kwenye hizi juhudi za kuinua soka letu!

Ukitaka kujua vilabu hivi viwili vya mchezo wa soka vina nguvu gani kwa Tanzania, inabidi nitoe mfano mmoja ninaoujua. Mmoja wa marais wastaafu wa Tanzania alipata kuniambia kwamba hakuna namna ambayo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Tanzania inaweza kupangwa katika siku ambayo kuna pambano la Watani wa Jadi.

Inajulikana kwamba wakati Simba na Yanga zinapocheza, Tanzania karibu yote husimama. Kuliko chama cha siasa au dini nyingineyoyote, hakuna taasisi inayoweza kujidai kuwa na ufuasi ambao vilabu hivi vinao. Vilabu hivi vinakusanya masikini na matajiri, vijana na wazee, wanawake na wanaume, watu wa rangi, dini na makabila yote wanashabikia timu hizi.

Timu hizi mbili zimeshiriki katika kujenga umoja na amani miongoni mwa Watanzania. Kwenye kushabikia timu hizi mbili, hakuna ubaguzi au tofauti ya aina yoyote na wala hakuna klabu mojawapo ya hizo inayoweza kufungamanishwa na dini, dhehebu au chama chochote cha siasa.

Misri wanajivunia vilabu vya Al Ahly na Zamalek lakini kuna itikadi za siasa ndani yake ambazo unaweza kuziunganisha na vilabu hivyo viwili jambo ambalo ni tofauti na Simba na Yanga ambazo ziko kwenye miji yote, dini zote, vyama vyote na miongoni mwa watu wa rangi zote.

Kwa hiyo, Rais mstaafu, Jakaya Kikwete na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe wanaweza kuwa na itikadi tofauti kisiasa lakini kwenye Yanga wanakuwa kitu kimoja. Inawezekana Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wanapishana kisiasa lakini linapokuja suala la Simba, wanakuwa kitu kimoja.

Si sawa na Kenya ambako Gor Mahia inahusishwa moja kwa moja na watu wa kabila la Wajaluo au AFC Leopards na kabila la Waluhya.

Taasisi hizi mbili ni miongoni mwa nguzo kubwa ya ndoto ile inayoitwa Tanzania.



# Mbaraka Mwinshehe bado kipenzi cha wana Morogoro

## >>> Aliwaachia alama ambayo ni vigumu kufutika
## >>> Nyimbo 'Tambiko la Wahenga, ni uthibitisho tosha

**Na Mwandishi Wetu**



**Mbaraka Mwaruka Mwinshehe**

BILA kujali kama Mbaraka Mwaruka Mwinshehe hivi sasa hayupo duniani, ajabu ni kwamba hadi leo huwaambii kitu wenyeji wa Morogoro hasa wakikumbukia mambo mengi mazuri aliyoyafanya enzi zake akiwa hai.

Mbaraka alifikwa na mauti mwaka 1979, ambapo gari alilokuwa akisafiria na wanamuziki wenzake waliokwenda Kenya kurekodi na kutumbuiza, liligongwa kisha yeye akafariki baadaye hospitalini kule Nairobi Kenya.

Lilikuwa ni basi la abiria ambalo mwanamuziki huyo alikuwa amepanda lilielezwa na Askari wa Usalama wa Barabarani (Traffic) kuwa, lilikuwa kwenye mwendo mkali kwenye Barabara Kuu ya kutoka Mombasa kuelekea Nairobi, wakati Mbaraka akienda kurekodi albamu yake mpya.

Katika msafara huo, pia Mbaraka alikuwa ameongozana na kundi la wanamuziki wa bendi yake ya Super Volcano, akiwemo shemeji yake Bonzo Kwembe ambaye alikuwa akipiga gitaa la besi.

Hadi sasa ushahidi unadhihirisha kuwa jina la Mbaraka bado linakumbukwa mno na Watanzania lakini zaidi, wenyeji wa Mkoa wa Morogoro hasa wa kabila la Waluguru ambako mke wa Mbaraka alikuwa 'shombe' kutoka kabila hilo.

Uelekeo ambalo wiki hii lilifanya ziara ya 'Mji Kasoro Bahari' limejionea jinsi ambavyo hadi leo hii yapata miaka 45 tangu kifo cha gwiji huyo kitokee, lakini wenyeji wa mji huo wangali wanamkumbuka kipenzi wao.

Uelekeo ambalo lilizugumza na wadau mbalimbali hasa wale wa muziki wa dansi; wengi wao wamekiri kuwa licha ya mkoa wao kujaliwa kuwa na hazina ya wanamuziki wengi; wakiwemo marehemu Salum Abdallah, Juma Kilaza na wengineo wengi, lakini kwa upande wa wana Morogoro wao wanadai Mbaraka Mwinshehe ndiye bado alama yao kuu.

Kwa mujibu wa mazungumzo ambayo Uelekeo liliyafanya baina yake na mpenzi aliyejitambulisha kwa majina ya Maneno Kilimo, yeye amekiri akisema Mbaraka atabakia kuwa kipenzi cha wana Morogoro.

Maneno ambaye ni mkazi wa Forest Hill, amesema licha ya yeye kutobahatika kumuona ana kwa ana Mbaraka, lakini ameongeza kuwa alianza kusikia sifa zake tangu akiwa bado mdogo.

Maneno ambaye ni mwajiriwa wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) ameongeza kuwa, wakati Mbaraka anafariki dunia, yeye alikuwa na umri wa miaka mitatu.

Amesema, licha ya kutomuona nguli huyo kutokana na utoto, lakini kila mara alikuwa akiwasikia ndugu zake na hata wazazi wake ambao walikuwa wapenzi wa muziki hasa ule wa dansi, wakilitaja jina la Mbaraka ambalo bado lingali vichwani mwao.

James Mkude aliyeishi maeneo ya Misufini, yeye amesema anashukuru kwamba kutokana na umri aliokuwa nao hadi Mbaraka anakufa, alikuwa amekwishabahatika mara kadhaa kumuona ana kwa ana akiwajibika kwenye majukwaa mbalimbali.

Mkude amesema wakati huo yeye alikuwa mpenzi wa kumbi nyingi za mji huo ambapo bendi ya Morogoro Jazz iliyobadilishwa jina kuwa Super Volcano ilikuwa ikitumbuiza wakazi wa mjini Morogoro.

"Mimi wakati Mbaraka anakufa, tayari nilikuwa na umri wa miaka 23.

Hivyo, kuna wakati nilikuwa napenda sana muziki wa mwanamuziki huyo. Kwa mfano, nilipokuwa nasikia kwamba Mbaraka atapiga kwenye Ukumbi wa Bwalo la Utamaduni ama Ukumbi wa Jeshi, nilikuwa mmoja wao", Mkude amekaririwa akitamba.

Ueleekeo ili kutaka liambiwe mengi yanayomhusu Mbaraka, lilifunga safari kiguu na njia hadi likatinga viunga vya Shule ya Msingi ya Mwembesongo.

Eneo hilo ndilo linalotajwa na wenyeji wa sehemu hiyo kuwa ndiyo ulikuwa ni mtaa aliokuwa akiishi Mbaraka.

Mwanamama Sheba Athumani Jongo (59) amesema anamkumbuka Mbaraka kutokana na tabia yake ya kupenda kuongea na watu hususan wale ambao walikuwa wakiishi naye mtaa mmoja.

Sheba ambaye ni mwalimu mstaafu wa Shule ya Mwembesongo aliliambia 'Jicho la HOJA' kuwa wakati Mbaraka anafariki, yeye alikuwa na miaka 21.

Bibi huyo ameongeza licha ya kufanya kazi yake ya ualimu akiwa bado msichana mbichi, lakini kwake wala ualimu haukuwa unamzuia kupata muda wa kuzisikiliza nyimbo za Mbaraka hasa alipokuwa amekwishamaliza majukumu yake.

Mwaka 1972, Mbaraka akiwa na bendi yake ya Morogoro Jazz aliipua albamu yake iliyokwenda kwa jina la 'Tambiko la Wahenga'.

Wimbo huo ambao aliutunga mahususi kwa ajili ya kuwaenzi Machifu wa Makabila ya Morogoro, ulitoka sambamba ukiwa na nyimbo nyingine kama vile, 'Njooni Mjionee Milima ya Uluguru Inavyotiririka Maji Safi', 'Taifa Stars Hoyee', 'Kombaini ya Morogoro', 'Akula Mwembesongo' na zingine kemkem ambazo zilikuwa gumzo kila kona ya mji.

Mbaraka enzi za uhai wake alikuwa ni miongoni mwa wanamuziki waliojaliwa kuwa na vipaji vingi.

Alijua kucharaza gitaa la solo, kutunga nyimbo na hata kuimba akiwakuna vilivyo wana Morogoro kufuatia kuimba kwa ustadi mkubwa wimbo wa 'Tambiko la Wahenga'.

Wimbo huo unakumbuka kazi nzuri ambazo zilifanywa na Machifu ama 'Vingalu' (kwa lugha ya Kiluguru) ambapo Mbaraka amesifia Machifu wa kabila la Waluguru, Wapogoro na Wakutu.


Aidha, Mbaraka katika wimbo wake huo hakuacha kuwasifu wenyeji wa maeneo ya Mgeta, Matombo, Ifakara, Mindu, Kingoluwira akiwaimba kwa kuwaeleza kuwa ni watu walio wakarimu kupindukia.

Chimbuko la mwanamuziki huyo kwa kabila ni Mzaramo ambaye alizaliwa kijiji cha Mzenga.

Akiwa na umri wa miaka ishirini mwanamuziki huyo alizamia moja kwa moja Morogoro ambapo alifanya makazi yake hadi alipokufa.



## Kona ya Urembo



Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219

# Vaa nguo rahisi

ISIPOKUWA mtindo ndio njia yako ya ubunifu, kufikiria nini cha kuvaa haipaswi kuhodhi asubuhi yako. Maamuzi kuhusu mavazi, viatu, vifaa, na mapambo sio lazima kuchukua muda mwingi wa maisha yako. Kuchagua na kudumisha WARDROBE rahisi sio lazima kuwa kazi na sio lazima kukuacha na mambo ya upweke tu kwenye chumbani yako.

Inachoweza kufanya ni kurahisisha kubeba matukio yako yajayo kwa taarifa ya muda mfupi, kutumia muda mfupi kusafisha, kukandamiza na kutunza nguo zako, na kustahimili mifadhaiko machache unapojaribu kufahamu cha kuvaa.

Je, huna mambo bora ya kufanya? Labda baadhi ya maduka ya ubunifu unayotaka kuchunguza? Labda ungefurahia dakika chache za ziada za kulala kila siku? Wakati wa kutafakari au kufanya mazoezi kila asubuhi? Acha kutumia muda wako wote kuandaa, kudumisha na kuamua nini cha kuvaa. Acha kutumia bajeti yako kwa kuongeza zaidi, ili tu ufurahie kuvaa kidogo.

Anza kutupa juu ya kitu kutoka chumbani yako (hicho HUTOKEA tu kuwa ya ajabu, ya starehe, ya kupendeza na ya utunzaji rahisi). Kisha, furahia siku yako.

**Nini cha Kufanya na nguo zako za ziada**

Uza nguo zako Kwa hivyo umepunguza kabati lako. Umeondoa kila kitu ambacho hakiendani kikamilifu. Umeondoa nguo hizo ambazo ni za kupendeza.

**Ununuzi wa biashara kwa soksi**

Ndiyo, kabati langu la nguo linaweza kuwa dogo kwa hatua nyingi, lakini soksi zangu… vizuri huwa bora kila wakati. Ninachukua soksi za kufubaisha.









> **INACHOWEZA kufanya ni kurahisisha kubeba matukio yako yajayo kwa taarifa ya muda mfupi, kutumia muda mfupi kusafisha, kukandamiza na kutunza nguo zako**

**Ninapenda rangi inayovutia.**

Kudumisha WARDROBE yangu ndogo

Mambo yanabadilika nina furaha kuripoti kwamba tangu nianze safari yangu ya kuvaa nguo ndogo, nimepungua uzito. UZITO mwingi. Nina uzito wa pauni 37.

**Kuishi Rahisi: Kunitunza bora ndani na nje**

Safari ya kurudi kwenye afya njema ni ya taratibu Kuchukua wakati na bidii kunitunza - ndani na nje - kama mfalme ama malkia.

**Kuweka Skinny Jeans? Ugumu wa kutupa nguo? Mimi pia.**

Nimesoma nakala nzuri kwenye Sparkpeople. Ilizungumza juu ya jinsi kuweka hizo "jeans za ngozi" kwenye kabati lako kwa mpangilio mzuri na mchache.SI kukuhimiza kupunguza uzito. Ilisema mazoezi ya kuhodhi nguo ili kuingia ndani inaweza kuumiza maendeleo yako ya kupunguza uzito. Nenda takwimu.

Hiyo ilikuwa ya kuvutia na ina maana (kujithamini chini, kujishusha kila wakati unapoangalia chumbani, kukataa kuona kwamba umri na uzazi hubadilisha uwiano wako).

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Aprili 03 - 09, 2024 |

## Aziz Ki mchezaji bora Machi



**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC, Yanga, Aziz Ki ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi Machi.

Aziz Ki amewashinda Feisal Salum na Clatous Chama katika katiba kinyang'anyiro hicho cha mwezi Machi.

Aziz Ki amefunga mabao 3 na kuhusika na mengine 4 hivyo kuhusika kwenye mabao 7 huku Yanga ikishinda mechi 3 Kati ya 4 iliyocheza mwezi Machi. 5-0 dhidi ya Ihefu, 1-0 dhidi ya Geita, 3-1 dhidi ya Namungo na kupoteza 2-1 dhidi ya Azam FC. Yanga SC ikaendelea kukalia kiti chake cha uongozi kwa mwezi wote wa Machi, imekusanya alama 9 katı ya 12.

Azam FC imeshinda mechi 2 katı ya 3 na kutoka sare 1 ikikusanya alama 7 katı ya 9, hivyo kocha wake Bruno Ferry amemshinda Miguel Gamondi. Azam iliifunga Yanga 2-1, ikaichapa Dodoma Jiji 4-1 na kutoka sare 1-1 na Coastal Union, hali iliyoibakisha kwenye nafasi yake ya pili kwenye msimamo.

Yanga SC wameshikilia nafanya yao ya kwanza kwa mwezi Machi na Azam FC wameshikilia nafasi yao ya pili kwa mwezi Machi.

## Roy Kean amshangaa Haaland



**MANCHESTER, Engaland**

BAADA ya mshambuliaji Erling Haaland wa Manchester City kushindwa kufua dafu mbele ya mabeki wa Arsenal kwenye mchezo wa Ligi Kuu England mwishoni mwa wiki iliyopita, jambo hilo limemuibua nahodha na kiungo mtukutu wa zamani wa mahasimu wao Manchester United, Roy Kean na kumkosoa vilivyo mfumania nyavu huyo mahiri.

Keane amedai kuwa, Haaland alicheza katika mechi hiyo kama mchezaji wa ligi daraja la pili la nchi hiyo (League Two) baada ya kushindwa kufanya kitu cha maana uwanjani katika mechi ambayo alipaswa kupambana na kuonyesha ubora wake na kuisaidia timu yake kwenye mbio za ubingwa.

## CRDB mdhamini mpya Kombe la FA

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF) limeingia mkataba na Benki ya CRDB wa miaka mitatu na nusu kudhamini michuano ya Kombe la Shirikisho (FA) wenye thamani ya shilingi bilioni 3.76.

Kwa kuanzia msimu huu CRDB watatoa dola laki moja sawa na shilingi milioni 255.

Na kwa sasa Kombe la FA litaitwa Kombe la Shirikisho la CRDB badala ya Kombe la Shirikisho la Azam kama ilivyokuwa awali.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari TFF imetoa mchanganuo wa kiasi hicho cha shilingi bilioni 3.76 kuwa ni pamoja na makato ya kodi ya Serikali.

# Simba, Yanga haijaisha mpaka iishe

## >>>Benchikha atamba kupindua meza ugenini

## >>>'Wananchi' kuwaduwaza Masandawana bila Yao



**Na Valensi Mbaga**

LICHA ya kutopata matokeo mazuri wakiwa hapa nyumbani, wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga bado zina matumaini ya kufanya vizuri katika mechi za marudiano ugenini.

Simba SC waliopoteza dhidi ya Al Ahly kwa kukubali kichapo cha bao 1-0, sasa wana kibarua kizito pale nchini Misri katika mchezo wa mkondo wa pili wakiwa ugenini utakaopigwa siku ya Ijumaa katika dimba la Cairo International.

Kocha wa Simba Abdelhak Benchikha amesemakuwa, licha ya kikosi chake kupoteza mchezo wa awali hapa nyumbani amejinasibu kwamba bado ana matumaini na viajana wake kwani walicheza vema na kilichowaangusha ni kutokutumia nafasi nyingi zilizotengenezwa ambazo amedai kama mastaa wa timu hiyo wangekuwa na utulivu basi ingetoka na ushindi mnono nyumbani mbele ya mabingwa hao watetezi wa Afrika.

"Malengo ni yale yale ya Simba kwenda nusu fainali, ni kweli tumepoteza kutokana na makosa yetu wenyewe. Washambuliaji walikosa umakini kutupia mipira nyavuni. Tunaenda kuzungumza na wachezaji hao na kurekebisha kila kitu ili tupate matokeo mazuri ugenini," ametamba Benchikha.

Kwa upande wa watani zao Yanga wao karata yao ya kwanza dhidi ya Mamelodi Sundowns ilitamatika suluhu wakiwa nyumbani, hivyo mchezo wao wa mkondo wa pili utakaopigwa kule nchini Afrika Kusini ni kama fainali kwa upande wao.

Licha ya kuwakosa mastaa wake baadhi katika mchezo huo wa kwanza bado Yanga SC walionyesha ubora wa hali ya juu dhidi ya mabingwa hao wa AFL, na katika mchezo huo wa pili Pacome pamoja na Aucho wanatarajiwa kucheza huku Attohoula Yao Kouassi kukiwa hakuna uhakika wa kucheza kutokana na daktari wa timu ya Yanga kusema kwamba bado hawajawa fiti barabara.

Beki huyo wa kupanda na kushuka wa kikosi hicho cha 'Wananchi', akiikosa tena mechi hiyo ya marudiano dhidi ya Mamelod itakuwa mara ya pili kufuatia kuikosa ile ya kwanza hapa nyumbani kwa sababu ya hayo majeraha aliyoyapata kwenye mechi ya Ligi Kuu ya NBC Yanga ilipocheza na Azam FC na kupoteza kwa bao 2-1.

Yanga SC wameshafika nchini Afrika Kusini tayari kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo wa marudiano utakaopigwa siku ya Ijumaa katika uwanja wa Loftus Versfeld.

Mabingwa hao wa soka nchini wanahitaji kupata ushindi wa aina yoyote ama kulazimisha sare ya magoli ili kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa barani Afrika.

Hakuna kisichowezekana, wakongwe hao wa soka la Tanzania wakijipanga vema wanaweza kuweka historia mpya kwa taifa kuona wawakilishi wake wote wakiingia hatua ya nusu fainali ya Ligi hiyo ya Mabingwa Afrika.

